**MSUYA** amdokeza Askofu Malasusa mrithi wa Dk. Sendoro
UKURASA 9

**WAANDISHI** wa IPP Media wapenya orodha wateule tuzo za EJAT 2023



UKURASA 8

**BILIONEA FAYED:** Afariki umri miaka 94, kashfa ubakaji wafanyakazi wake zamwandama



UKURASA 14



**DE BRUYNE HATIHATI KUIVAA ARSENAL**
UKURASA 21


# Nipashe

Ijumaa Septemba 20, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581805

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Jaji Warioba aonya mwelekeo wa siasa

Mbowe naye alia na mwezi wa maombolezo CHADEMA...
*Ukurasa wa 2*



Jaji Warioba Mbowe



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto) akiweka jiwe la msingi katika mradi wa Kufua Umeme Mto Malagarasi MW 49.5, mkoani Kigoma. Kulia ni Mkuu wa mkoa huo, Thobias Andengenye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko azindua mradi umeme unaookoa bil. 19/- kila mwaka

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

HISTORIA imeandikwa Kigoma baada ya kuwekwa jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa kuzalisha umeme katika maporomoko ya Malagarasi ambao utauwezesha mkoa kupata umeme wa gridi ya taifa.

Mbali na mradi huo, Kigoma pia itaanza kupata umeme wa gridi ya taifa katika njia zingine hali itayowezesha kufungua zaidi mkoa kiuchumi. Umeme utakaozalishwa katika mradi huo utakuwa wa Megawati 49.5.

Sambamba na mradi huo, pia limewekwa jiwe la msingi katika kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme katika eneo la Kidahwe, wilayani hapa.

Akizungumza jana baada ya kuweka mawe hayo ya msingi, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alisema hatua hiyo imeandika historia mpya katika mkoa wa Kigoma.

Dk. Biteko alisema kutokana na hatua hiyo, Kigoma, moja ya mikoa

**Endelea** Uk. 3

UKURASA WA 6

## JAMII ISIWE CHANZO KUSABABISHA MAGONJWA AFYA YA AKILI

WATAALAMU bingwa na bobezi wa magonjwa, afya ya akili na mfumo wa fahamu, kutoka Hospitali ya Taifa...

UKURASA WA 15

## SERIKALI, TLS WAKUTANA WAJADILI KATIBA MPYA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi na Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili wa Tanzania...

## ACT yatoa mbinu tatu kumaliza migogoro w'biashara na serikali

UKURASA 5

**MICHEZO** **AL AHLI TRIPOLI WAKODI MABAUNSA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA

# Warioba aonya mwelekeo wa siasa nchini

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba ametahadharisha siasa nchini iko katika mwelekeo mbaya.

Amesema kuwa kwa miaka mingi Uchaguzi wa Serikali za Mitaa umekuwa unasimamiwa na serikali na umekuwa huru na haki, lakini alichokishuhudia mwaka 2019 ni kama nchi inarejea kwenye mfumo wa chama kimoja.

Vilevile, ametoa angalizo kuwa siasa imegeuka kutoka kutoa hoja na kukosoana kwa lengo la kujenga nchi, hivi sasa anaona siasa za ukabila na udini.

Jaji mstaafu Warioba aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wa Kituo cha Demokrasia (TCD) na wadau waliokutana kujadili tathmini ya hali ya demokrasia nchini mkoani Dar es Salaam jana.

Alisema Uchaguzi wa mwaka huu wa Serikali za Mitaa utakuwa na umuhimu mkubwa kulinda amani ya nchi, akishauri kufanyike tathmini ya utawala bora na demokrasia.

"Mjue uchaguzi wa mwaka huu utakuwa na umuhimu mkubwa kwa amani ya nchi yetu. Lazima tutafute njia ambayo itafanya sote tutaridhika.

"Bado mpaka jana nilikuwa ninajitahidi, bado muda mfupi tunakwenda Uchaguzi wa Serikali za Mtaa, tutafakari viongozi wote tunaohusika tukubaliane, tutakapokwenda katika uchaguzi tuwe tumekubaliana, la sivyo tukienda na mapambano haya, yanaweza kujenga misingi ya vurugu katika nchi yetu.

"Mambo ya msingi ndiyo yanayosababisha vurugu na tusisahau tuna uzoefu katika nchi hii yaliyotokea Zanzibar mwaka 2001, tusije tukafika katika hali hiyo," alionya.

Jaji Warioba aliongeza: "Siku hizi ukizungumzia demorasia ndani ya Tanzania ni kama unazungumzia ilianza miaka 30 iliyopita baada ya mfumo wa vyama vingi, ninadhani hapo tunakosea, tuanzie mbali zaidi.

"Katiba inasema msingi wa madaraka na mamlaka ni wa wananchi (Ibara ya 8 ya Katiba ya nchi), kimsingi unapozungumzia demokrasia unazungumzia wananchi. Katika tathmini tuangalie wananchi wamefaidika vipi," alisema.

Jaji Warioba alisema wao walioishi wakati wa ukoloni, hakukuwa na demokrasia, na sasa wanazungumzia uhuru wa kutoa mawazo, kusikika, mikutano ya hadhara na maandamano.

"Wakati ule hakukuwapo hivyo, wakati wa wakoloni pamoja na sasa ndio wale ambao walikuwa hapa wakaona demokrasia hapa haifai, sasa ndio wamekuwa mafundi wa kutufundisha demokrasia.

"Tujiulize mnapofanya tathmini wananchi wana haki ya kuchagua wawakilishi wao? Eneo moja mngefanya utafiti mwone wananchi wanaonesha vipi, mwone wanavyojitokeza kupiga kura.

"Mwangalie wakati wa mfumo wa chama kimoja wakati wa uchaguzi wananchi walikuwa wanajitokeza kwa wingi 2019/20 ilikuwa ajali, haikuwa katika utaratibu wa kawaida wa mchakato wa uchaguzi.

"Kila uchaguzi una dosari, hakuna unaoweza kupita bila dosari, lakini mawakala walisambaratishwa wengi tu, hata upigaji kura wenyewe halikuwa jambo la kawaida."

Alisema kuwa hivi sasa anadhani ugomvi mkubwa ni waliosimamia uchaguzi 2019/20 ndio wataendelea kusimamia.

"Wanaaminika? Ninajiuliza, ukichukua mfano Serikali za Mitaa, tangu wakati wa chama kimoja hadi mfumo wa vyama vingi, uchaguzi huu ulisimamiwa na serikali.

"Mwaka 1994 ulisimamiwa na serikali, 1999, 2004, 2009, 2014, mara tano tumefanya Uchaguzi Serikali za Mitaa ukisimamiwa na serikali, kulikuwa na dosari za hapa na pale, lakini kwa ujumla ulikuwa wa haki na huru, na katika kipindi kile hata vyama vya upinzani vilishika vijiji.

"Lakini 2019 inabadilika kabisa, mwisho unakuta kama tumerudi mfumo wa chama kimoja. Kwanini ilitokea hivyo? Ninadhani hayo.

"Mimi isingenipa tatizo, nimekuwa nikitetea mabadiliko ya katiba lakini bado niliamini tungeweza kufanya uchaguzi huru na haki, lakini sasa hivi ni ngumu," Jaji Warioba alisema.

Waziri Mkuu mstaafu huyo aliweka wazi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na timu yake walifika nyumbani kwake kumsalimia na akajaribu kuwashawishi waahirishe maandamano.

Alisema kuwa aliwatafuta na upande wa pili, Chama Cha Mapinduzi (CCM), akawaambia amekaa na CHADEMA wamemweleza wasiwasi wao na ni vizuri washughulikiwe, akihakikishiwa uchaguzi utakuwa huru na haki.

Alisema aliona matukio likiwamo la Mbeya, akajiuliza "Msajili wa Vyama vya Siasa ni mlezi wa vyama, hakuna njia ya mashauriano na kuleta suluhu?"

Jaji Warioba alisema kuwa hivi sasa kwa lugha wanayozungumza, imefikia wananchi kuona ni mtu mmoja tu mwenye uwezo wa kufanya kila kitu, hata vijijini waandishi wa habari wakienda kuzungumza nao, wanasema tunaomba Rais atuangalie kwa jicho la tatu.

"Tunafundisha demokrasia au usultani na ufalme? Ninadhani tathmini hizi tuzifanye. La mwisho, umoja na amani ya nchi; demokrasia katika nchi hii ni lazima uimarishe umoja na amani yetu, kama hailindi amani na umoja haitufai," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Bernadetha Kafuko, akizungumza katika kongamano lililoandaliwa na kituo hicho jijini Dar es Saalam jana kuadhimisha Siku ya Demokrasia Duniani ambayo hufanyika kila mwaka Septemba 15. **PICHA: BLOGU YA MICHUZI**

**MBOWE, LISSU**

Mwenyekiti wa TCD, Mbowe, alisema mwezi Septemba umekuwa wa maombolezo kwa CHADEMA, akiwashukuru Watanzania wote, vyama vyote na taasisi mbalimbali ambao wamelia nao.

"Kwetu ulikuwa mwezi mgumu mno, tunapata wakati mgumu kutafakari namna ya kufanya wajibu ulio bora ndani ya TCD na wakati huo tukilia kwa madhila tunayopata.

"Ili demokrasia iwe na maana lazima itambue haki. Ili kuwa na demokrasia kwa taifa, lazima kuwe na utashi wa kisiasa na unatakiwa utoke kwa waliopewa dhamana kuongoza taifa," alisema.Alisema wamepoteza wenzao na kuendelea kutokujua wanachama na viongozi wenzao waliko. "Nitambue katika mkutano huu, kumekuwa na upotevu wa viongozi wetu katika mazingira ya kutatanisha. Tumeomba serikali ituambie wako wapi, nao wanasema hawajui wako wapi. Basi sintofahamu inabaki kwa taifa zima," alisema.

"Mnategemea taasisi mliyoisajili ifanye shughuli za kihalali za kisiasa ifanye nini? Tuna deni la roho za watu," alisema Mbowe.

Katika mkutano huo, Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle, alisema siku zote nchi yake imewekeza kwa watu na demokrasia, hivyo wanathamini mchakato wa demokrasia unaowahusu watu moja kwa moja.

Alisema siku za hivi karibuni kuelekea katika uchaguzi, Tanzania na Marekani zimekabiliwa na vurugu ambazo zinatishia mchakato wa demokrasia katika mataifa hayo.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, alisema kitu pekee kilichobadilika na cha maana kwa mtazamo wake katika sheria mpya ni kwamba, badala ya wagombea waliokuwa wanapita bila kupingwa, sasa sheria inasema wakienguliwa wakabaki peke yao, watapigiwa kura ya ndio au hapana.

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema: Yaliyotokea mwaka 2001 walipoitisha maandamano ya amani na watu kadhaa kupoteza maisha, hayapaswi kujirudia. Prof. Lipumba alisema maoni ya Jaji Warioba aliyotoa ni muhimu na kwa kuwa vyombo vya dola vipo, kuna haja kufanya mazungumzo na majadiliano ili mambo yasiharibike zaidi kuliko yalivyo sasa.

Viongozi wengine waliohudhuriwa mkutano huo ni Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Charles Kitima.

Wengine ni Askofu wa Kanisa la Uamsho la Moravian Tanzania, Emmaus Mwamakula na Katibu Mkuu wa Shura ya Maimam Tanzania, Shehe Issa Ponda.

# Mapya yaibuliwa tukio watu watatu kuuawa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BABA wa familia ya watu watatu waliouawa na watu wasiojulikana katika Kata ya Nala, jijini Dodoma, Robert Mugema ameomba serikali kuimarisha ulinzi katika mtaa lilikotokea tukio hilo kwa kuwa kuna hofu.

Amesema kuwa siku watoto wake wanauawa, kuna taarifa kwamba baadhi ya nyumba za mtaa huo zilifungwa milango kwa makufuli.

Septemba 16, mwaka huu, nyumbani kwa Mugema, waliuawa watu watatu ambao ni Milcah Robert (12), Fatuma Mohamed (20) na binti wa kazi, Makiwa Abdallah (16) huku mama wa familia hiyo, Lusajo Mwasonge (40) akijeruhiwa na kulazwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Akizungumza juzi nyumbani baada ya ibada ya kuaga mwili wa binti yake, Mugema alisema anakwenda mkoani Geita kwa ajili ya mazishi ya aliyekuwa mfanyakazi wake wa ndani, lakini familia yake itabaki katika nyumba hiyo.

Hivyo, aliomba Serikali ya Mtaa, wilaya na mamlaka zote za ulinzi na usalama waendelee kuimarisha ulinzi mahali hapo kwa sababu bado hana imani.

"Nina roho ya ujasiri ndani yangu lakini mwili wangu ni dhaifu sana, mnaponiona nalia si kuwa siwasikii mnaponihamasisha niwe imara. Moyoni mwangu niko imara kabisa lakini mwilini kwangu ni dhaifu sana, niwaombe kuimarishwe ulinzi katika maeneo ya Segu Bwawani.

"Wakati wa tukio kuna baadhi ya majirani nyumba zao zilifungwa kwa makufuli, maana yake eneo hili haliko salama au halikuwa salama. Simlaumu mtu wala kumtaja yeyote lakini Mungu awabariki kwa mkono wake," alisema.

Awali, akitoa mahubiri katika ibada ya kuaga miili, Askofu wa Kanisa la The Gospel Special Message Ministry (Gome), Majid Salim Ally, alisema tukio hilo ni baya na hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa kama ilivyo kwa matukio mengine.

"Uovu unaangamiza nchi na ninatamka sasa hawa waliofanya tukio hili wakamatwe kwa jina la Yesu, niombe serikali iongeze nguvu kwenye vyombo vya ulinzi na usalama wasipewe taarifa na kukaa nazo bila kuzitendea haki," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Segu Bwawani, Jeremiah Mulima alisema Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri alifika eneo la tukio na kuwaomba wananchi kuwa watulivu na kusubiri tamko la polisi ngazi ya wilaya na mkoa.




Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT 2023 Ernest Sungura (kulia), akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za MCT Tegeta, Dar es Salaam jana kuhusu kukamilika kwa majina ya wateule wa tuzo hizo. Kushoto ni Mwenyekiti wa Jopo la Majaji, Halima Shariff. **Habari Uk. 8. PICHA: MIRAJI MSALA**

# Biteko azindua mradi umeme unaookoa bil. 19/- kila mwaka

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

HISTORIA imeandikwa Kigoma baada ya kuwekwa jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa kuzalisha umeme katika maporomoko ya Malagarasi ambao utauwezesha mkoa kupata umeme wa gridi ya taifa.

Mbali na mradi huo, Kigoma pia itaanza kupata umeme wa gridi ya taifa katika njia zingine hali itajayowezesha kufungua zaidi mkoa kiuchumi. Umeme utakaozalishwa katika mradi huo utakuwa wa Megawati 49.5.

Sambamba na mradi huo, pia limewekwa jiwe la msingi katika kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme katika eneo la Kidahwe, wilayani hapa.

Akizungumza jana baada ya kuweka mawe hayo ya msingi, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alisema hatua hiyo imeandika historia mpya katika mkoa wa Kigoma.

Dk. Biteko alisema kutokana na hatua hiyo, Kigoma, moja ya mikoa ya pembezoni, sasa itageuka kuwa kitovu cha nishati na itakayofanya mkoa kupiga hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alisema umeme huo na ule wa kutoka vyanzo vingine vya gridi ya taifa, vitafanya Kigoma kuwa na umeme wa uhakika ambao utachochea kasi ya maendeleo.

"Kigoma sasa itafunguka kimaendeleo kwa sababu ya umeme wa gridi ya taifa. Baada ya kufunguka kwa miundombinu ya usafiri, sasa ni zamu ya kufunguka kwa umeme na hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kasi ya maendeleo katika nyanja mbalimbali.

"Enzi zile kabla ya barabara za lami, haikuwa shida ukiwa Mwanza au Dar es Salaam kumtambua mtu aliyekuwa akitoka Kigoma. Ulikuwa unamtambua kwa vumbi tu lakini sasa ni historia.

"Sasa umeme wa uhakika wa gridi ya taifa unaanza kuingia Kigoma. Ile historia ya kuwa moja ya mikoa iliyo nyuma kiuchumi inafutika. Tulianza na barabara, tunakuja na umeme hatimaye treni ya kisasa (SGR). Nuru inawaka Kigoma," alisema.

Naibu Waziri Mkuu Biteko alisema serikali imetoa Sh. trilioni 1.2 ambazo pamoja na ujenzi wa mradi wa Malagarasi, zitatumika kupokea, kupoza na kusafirisha umeme kutoka Nyakanazi kilovoti 620, ujenzi wa njia ya Tabora - Uvinza hadi Kigoma, Katavi hadi Uvinza kilovoti 220 kwa ajili ya treni ya SGR.

Dk. Biteko alisema kuwapo umeme wa gridi ya taifa kutalipunguzia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) gharama za ununuzi wa mafuta mazito kwa ajili ya majereta yanayozalisha umeme. Kwa mujibu wa Dk. Biteko, kwa mwaka TANESCO hutumia Sh. bilioni 35 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta hayo kwa ajili ya kuzalisha umeme.

"Pamoja na kutumia fedha hizo, ukiangalia kiasi kinachopatikana kwa ajili ya kuuza umeme ni Sh. bilioni 16, hivyo shirika linapata hasara ya Sh. bilioni 19. Kwa hiyo ulikuwa mzigo mkubwa na sasa tutauondoa," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Boniface Nyamohanga, alisema Kigoma ilikuwa inapata Megawati 8.5 za umeme unaozalishwa kutokana na mafuta mazito na umeme wa jua Megawati 4.7 unaozalishwa na kampuni ya Next-Gen Solar.

Alisema umeme wa gridi ya taifa utalipunguzia mzigo shirika wa uzalishaji na kuwa na umeme wa uhakika ambao utachochea kasi ya ukuaji uchumi wa mkoa, maisha bora ya wananchi na Pato la Taifa.

"Umeme huu pia utasaidia kuboresha huduma za kijamii kama elimu na afya. Pia utatengeneza ajira za muda mfupi na mrefu. Zaidi ya wafanyakazi 700 wanatarajiwa kuajiriwa.

"Licha ya manufaa hayo, gharama za uzalishaji umeme zitapungua kwani tutaondoa majereta ambayo yalikuwa yakitumika kuzalisha umeme ambayo yalikuwa mzigo mkubwa kwa shirika," alisema.


**CO-OPERATIVE BANK OF TANZANIA (CBT)**

**NOTISI YA MKUTANO MKUU WA KWANZA WA CO-OPERATIVE BANK OF TANZANIA (CBT)**

TUNAPENDA KUWATAARIFU WANACHAMA NA WANAHISA KUWA MKUTANO MKUU WA KWANZA WA CO-OPERATIVE BANK OF TANZANIA UTAFANYIKA KAMA IFUATAVYO:

| | | |
|---|---|---|
| TAREHE | : | **17 OKTOBA, 2024** |
| SIKU | : | ALHAMISI |
| MUDA | : | **SAA 3.00 ASUBUHI** |
| MAHALI | : | UKUMBI WA GENERATION ULIOPO JIJINI DODOMA MAENEO YA KISASA. |

TUNAPENDA KUWATAARIFU ZAIDI KUWA DONDOO ZA MKUTANO ZITASAMBAZWA KWA WANACHAMA NA WANAHISA SIKU SABA KABLA YA TAREHE YA MKUTANO.

KILA CHAMA/TAASISI/KAMPUNI ITUME **MJUMBE MMOJA TU,** NA MWANAHISA BINAFSI ANAYO NAFASI YA KUHUDHURIA BINAFSI AU KUWAKILISHWA KWA MUJIBU WA MASHARTI YA BENKI.

KARIBUNI SANA,

John Rugambo,
**KATIBU WA BODI**

Tarehe: 19/09/2024

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# ADVERTISEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

## 1. POSITION: CAPTAIN - (30 POSTS)

### 1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:

- Must have flown with more than 3500 flying hours with an Airline Transport Pilot License, Multi Engine and Instrument Rating.
- Must have 1000 hours as a Pilot in Command and an experience of handling a minimum of 20 tons' equipment or above with a good performance.

### 1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- Responsible for safety of the aircraft, its occupants and cargo pre, during and post flight.
- Maintain a high standard of discipline, appearance, uniformity and promptness of Co-pilots and Cabin Crew.
- Determine the achievement of commercial aspects of flights safety is not impaired to obtain additional revenue load for the Company.
- Ascertain that Flight Plans, Notam, Fleet Notices, Weather and any pertinent documentation and service items that flight may require are briefed.
- Verify that the loading of aircraft being performed in accordance with laid down procedures.
- Report all incidents and accidents.
- Verify that all documents/certificates required being on board the aircraft are available and valid.
- Report any Flight delays of flights.
- Accept and sign for diplomatic mail, precious cargo and supervise stowage aboard the aircraft and handover to destinations.
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

## 2. POSITION: FIRST OFFICER - (4 POSTS)

### 2.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:

- Must have flown with more than 250 flying hours or above with Commercial Pilot License, Multi Engine with Instrument Rating.
- Must be with an experience of handling a minimum of 10 tons' equipment with good performance.

### 2.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- To participate in the Pilot-in-Command's crew briefing, and make himself aware of all relevant aeronautical and meteorological information as well as relevant papers documenting the aircraft technical status and its anticipated load.
- To prepare the OFP and when necessary, file the ATS Flight Plan with the appropriate Authority. If stored plans are used then he should ensure that the correct plan has been activated
- To carry out such duties concerning the flight in accordance with the SOP, including procedures, limitations and performance related to the specific aircraft type, as allocated to him by the Pilot-in-Command;
- To confirm the safe navigation of the aircraft, maintaining a continuous and independent check upon both the geographical position of the aircraft and its safe terrain clearance
- To safely and properly conduct the flight in compliance with the current flight plan and the Pilot-in-Command's instructions when the Pilot-in-Command is not at the controls. Any change to the current flight plan has to be notified to the Pilot-in Command.
- To provide advice, information and assistance to the Pilot-in-Command, as may contribute favorable towards the safe and efficient conduct of the flight.
- To assist the Pilot-in-Command in administration duties related to the flight and
- To seek and receive information and/or explanation from the Pilot-in Command, as may be necessary to enable fulfilment of functions.
- To assist the Flight Safety Department for all Technical related matters
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

## 3. POSITION: PUBLIC RELATIONS OFFICER II (1 POST)

### 3.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:

- Applicants must hold a Bachelor's Degree in one of the following fields: Public Relations and Advertising, Mass Communication, Journalism, Business Communication or an equivalent qualification from a recognized institution.

### 3.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES;

i. Assist in the routine public relations activities such as the writing of news and feature articles.
ii. Monitor media coverage related to Air Tanzania and provide daily reports.
iii. Capture high-quality photographs for use and maintain records of major events.
iv. Develop visually engaging graphic content, including digital banners, social media posts, infographics and promotional materials.
v. Develop, manage and update content for digital platforms, TV, Radio and the ATCL website.
vi. Draft press releases and organize press conferences.
vii. Assist in organizing and facilitating exhibitions, conferences, seminars and corporate events.
viii. Support the planning and execution of public relations campaigns.
ix. Support crisis communication efforts by ensuring prompt and effective messaging x. Perform any other official duty as may be assigned by your supervisor

## 4. TERMS AND CONDITIONS:

Ten (10) years contract for Tanzanian and with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

## 5. GENERAL CONDITION FOR APPLICANTS:

i. All applications must be sent through ATCL Recruitment Portal by using the following address: **https://recruitment.atcl.co.tz** and NOT otherwise. This address can also be found at Air Tanzania website.
ii. Interested applicants must upload a dully signed letter for consideration of the application. The letter should be addressed to Managing Director & CEO, **Air Tanzania Company Limited, P.O. Box 543, Dar es Salaam.**
iii. An updated curriculum vitae (CV),
iv. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
v. Name and address of at least two reputable referees;
vi. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.
vii. Only shortlisted candidates will be informed on a date for interview viii. Women are encouraged to apply.
ix. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.
x. Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

## HABARI KITAIFA

# Mchinjita atoa mbinu za kumaliza migogoro wafanyabiashara, serikali

## -Aguna fidia wananchi Bonde la Msimbazi

**Na Halfani Chusi**



MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo Bara, Isihaka Mchinjita (pichani) ameshauri serikali inaposanifu na kujenga barabara, itenge maeneo kwa ajili ya machinga kufanya biashara zao ili kumaliza migogoro ya wafanyabiashara na serikali.

Mchinjita alishauri hayo jana Karume, jijini Dar es Salaam alipozungumza na wananchi, ikiwa ni mwendelezo wa ziara zinazofanywa na viongozi wakubwa wa chama hicho waliojigawa kikanda.

Ushauri mwingine aliotoa ni kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya machinga katikati ya jiji ili kupunguza mwingiliano wa kibiashara.

Alisema hiyo itamaliza dhana ya kuonekana Kariakoo ni mahali pa mapambano kati ya wafanyabiashara na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Eneo la Kariakoo mizigo yake yote inatoka bandarini, serikali ilitangaze eneo la Kariakoo kuwa ni eneo huru la biashara. Hiyo itasaidia kuwaondoa maofisa wa TRA na huu mgogoro wa mara kwa mara hautatokea tena.

"Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeziba mwanya na kuondoa hali ya kuwindana na kuviziana kati ya wafanyabiashara na maofisa wa TRA," alisema Mchinjita.

Kuhusu wananchi wanaoondolewa katika Bonde la Mto Msimbazi kulalamikia kutolipwa fedha kulingana na thamani ya eneo, alitaka serikali kurejea upya kwa wakazi hao kutatua changamoto hiyo.

"Tunafahamu mradi wa Benki ya Dunia umetoa fedha zaidi ya Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kubadilisha sura ya Bonde la Mto Msimbazi, lakini wananchi wanalipwa fedha kidogo.

"Hata fidia wazolipa bado ni ndogo, kuna mama ameniambia yeye nyumba yake imebomolewa, analipwa fidia Sh. milioni 14 na hawajaambiwa kiwanja atapata wapi.

"(Sh.) milioni 14 ni fedha ndogo sana kwa kiwanja kilichopo katikati ya jiji wakati leo ukivuka tu hapo Kigamboni kabla ya Mji Mwema kiwanja ni zaidi ya Sh. million 30," alisema kwa ukali Mchinjita.

Alitaka serikali kurejea upya kinachoendelea katika bonde hilo na wananchi waliokataa kulipwa, waingizwe kama sehemu ya wanahisa ili wanufaike na mradi utakaojengwa.

Akizungumzia ongezeko la machinga, Mchinjita alisema limetokana na seriali kutokuwa na mipango mizuri ya kuajiri vijana, akisisitiza wengi wao ni waliohitimu vyuo vikuu na wakakosa ajira.

Mchinjita alisema takwimu zilizopo zinaonesha kuwa kila mwaka vijana 1,000,000 wanaingia katika soko la ajira, lakini serikali huajiri vijana 70,000 tu, hivyo 930,000 hukosa ajira kila mwaka.

Alisema hali hiyo imesababishwa na serikali kwa kutokuwa na ubunifu wa kuwawezesha vijana kupata ajira na kujiondoa katika lindi la umaskini.

Akihitimisha mkutano wake kwa kuwataka wananchi kuunga mkono chama chake kwa kuwachagua viongozi wao ili waje na mbinu mbadala za kufanye kile alichokiita "kukomboa nchi".

# Watumishi TASAF wanolewa ufuatiliaji, tathmini Zanzibar

**Na Faustine Feliciane**

BAADHI ya watumishi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wameshiriki Kongamano la tatu la Ufuatiliaji na Tathimini unaofanyika Zanzibar na kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtaalamu wa Masuala ya TEHAMA wa Mfuko huo, Peter Lwanda, alisema wanashiriki mkutano huo ili kujifunza na kuongeza ujuzi katika kufanya tathimini na ufuatiliaji.

"Kitengo kama hiki sisi TASAF tunacho muda mrefu, lakini kwa sababu tunafanya ufuatiliaji na kufanya tathmini kwenye miradi yetu mbalimbali, mkutano huu ni muhimu kwetu kuongeza ujuzi na kuendelea kujifunza ili kuwa na uhakika wa kufanya kazi kwa ufasaha," alisema Lwanda.

Alisema TASAF wamekuwa wanaendesha miradi mbalimbali Zanzibar na katika mkutano huo, walibainisha mafanikio yaliyofikiwa na walengwa wa mfuko huo visiwani Zanzibar.

"Lakini kwenye suala la tathmini, sisi pia tumekuwa tukijitathmini kwa kutumia wataalamu kutoka nje ya TASAF tukiamini hatuwezi kujitathmini kama tunataka matokeo sahihi, na kikubwa ni kuhakikisha malengo ya mfuko huu yanafikiwa katika kila miradi yake," alisema.

Mkutano huo ulianza Septemba 17 na kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali. Unafikia tamati leo visiwani humo.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# ADVERTISEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified experts to fill the position of Captain as detailed below: -

**1. POSITION: FOREIGN CAPTAIN - (10 POSTS)**

**1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Must have flown with more than 3500 flying hours with an Airline Transport Pilot License, Multi Engine and Instrument Rating.
- Must have 1000 hours as a Pilot in Command and an experience of handling a minimum of 20 tons' equipment or above with a good performance.
- Must be rated on one of the following aircraft type; B787, B737MAX and Q400 or Q300
- Must have a valid license
- Must be current and have a minimum or 500hrs on type as PIC.

**1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Responsible for safety of the aircraft, its occupants and cargo pre, during and post flight.
- Maintain a high standard of discipline, appearance, uniformity and promptness of Co-pilots and Cabin Crew.
- Determine the achievement of commercial aspects of flights safety is not impaired to obtain additional revenue load for the Company.
- Ascertain that Flight Plans, Notam, Fleet Notices, Weather and any pertinent documentation and service items that flight may require are briefed.
- Verify that the loading of aircraft being performed in accordance with laid down procedures.
- Report all incidents and accidents.
- Verify that all documents/certificates required being on board the aircraft are available and valid.
- Report any Flight delays of flights.
- Accept and sign for diplomatic mail, precious cargo and supervise stowage aboard the aircraft and handover to destinations.
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**2. TERMS AND CONDITIONS:**

One (1) year contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**3. GENERAL CONDITION FOR FOREIGN APPLICANTS:**

i. All applications must be sent through ATCL Recruitment Portal by using the following address: **https://recruitment.atcl.co.tz** and NOT otherwise. This address can also be found at Air Tanzania website.
ii. Interested applicants must upload a dully signed letter for consideration of the application. The letter should be addressed to Managing Director & CEO, Air Tanzania Company Limited, P.O. Box 543, Dar es Salaam.
iii. An updated curriculum vitae (CV),
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.
vi. Only shortlisted candidates will be informed on a date for interview
vii. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.
viii. Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii isiwe chanzo kusababisha magonjwa afya ya akili

**WATAALAMU** bingwa na bobezi wa magonjwa, afya ya akili na mfumo wa fahamu, kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, wameeleza namna ubongo wa binadamu unavyofanya kazi na kuhifadhi kumbukumbu.

Baadhi ya watu wanaopoteza kumbukumbu, wanaweza kusababishiwa na magonjwa ya akili kama vile msongo wa mawazo, lakini vilevile kupotea kwa kumbukumbu inaweza kuwa tiba muhimu kwa mwili wa binadamu.

Wanatoa mfano kuwa mtu anaposhuhudia mauaji ya kikatili huwa haitoki kwenye kumbukumbu yake na tiba itakayomfaa ni kupoteza kumbukumbu.

Bingwa Mbobezi wa Afya ya Akili na Mfumo wa Fahamu kutoka hospitali hiyo, Dk. Damas Mlaki, anatoa darasa kwa umma akisema jamii inapaswa kuzingatia elimu kuhusu afya ya akili, kwa manufaa ya ustawi wa jamii kwa ujumla.

Magonjwa yanayohusisha ubongo kutofanya kazi yake ipasavyo ni msongo wa mawazo pia kiharusi na waliojeruhiwa sehemu fulani ya ubongo kutokana na ajali na kukwamisha utendaji kazi ya ubongo ipasavyo.

Kadhalika, wapo ambao hupata athari hasa kupoteza kumbukumbu za masuala mbalimbali ambazo ubongo kwa mfumo wake thabiti, huzihifadhi kwa matumizi ya baadaye.

Msongo wa mawazo, sononа, watu kupitia na kuishi kwenye changamoto za maisha ambazo hazipati ufumbuzi wa mapema, huuathiri ubongo na kuhitaji kupewa matibabu ya dawa ama ushauri.

Mbinu za kujikinga na namna ya kufanya ubongo utunze kumbukumbu, inaelezwa kuwa ni kufanya mazoezi ya kimwili na kiakili, lishe bora na kupata usingizi wa kutosha usiopungua saa nane.

Inashauriwa watu kuzingatia usingizi ili kurejesha kumbukumbu na wanafunzi wanapewa angalizo la kutoa muda wa kujisomea kwa kuupumzisha ubongo kwa kupata usingizi jambo ambalo ni muhimu.

"Wanaokesha, wanafunzi kusoma bila kuupa nafasi usingizi ni tatizo. Wanaweza hata wanachokisoma wasikikumbuke katika chumba cha mtihani. Inahitaji ulale angalau saa nane kwa siku, ili kuzihuisha kumbukumbu."

Mbinu nyingine na kutunza kumbukumbu ni kuupa ubongo mazoezi ya kiakili, wataalamu wanasisitiza pia kuangalia filamu, kusoma vitabu, gazeti, kucheza michezo ya asili kama bao, kwa sababu mtu anatumia fikra ili kumshinda mwenziwe.

Witou kwa watu wote ni jamii izingatie ushauri wa wataalamu wa afya, ili kuboresha ustawi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.


Vilevile, jamii iache unyanyapaa kwa ambao uwezo wao wa ubongo na kutunza kumbukumbu ni duni hasa watoto, ambao wanapokuwa masomoni hushindwa kufikia wastani wa juu, kwa matamanio ya wazazi au walezi.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala, anasema jamii hasa familia, iache kufananisha uwezo wa ubongo baina ya mtoto mmoja na nduguze, kwani ni kawaida kutofautiana kutokana na ubongo ulivyoendelezwa.

Utafiti unaofanywa maeneo tofauti duniani unaonesha kuwa, uwezo wa ubongo kati ya binadamu mmoja na mwingine hutofautiana, licha ya kuwa pengine wana rika sawa hata kama watoto wa familia moja.

Jamii inatakiwa kuacha kumsema vibaya mtoto mwenye uwezo mdogo hata kumnyanyapaa na ni vyema ubongo wa watoto hao ukaanza kuendelezwa mapema ili kukuza nafasi ya kutunza kumbukumbu za wanachojifunza hata kukuza vipaji vyao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kila kukicha ukatili mama, mtoto tunahitaji staili mpya ukomeshaji

Na Sabato Kasika

**UKATILI** dhidi ya wanawake na wasichana ni sehemu ya ukiukwaji wa haki za binadamu, inazochangia kuathiri zaidi ya wanawake milioni 1.3 duniani kote.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake, UN Women, ambayo imewahi kuitoa na kusambazwa katika vyombo vya habari.

Kwa mujibu wa shirika hilo, majanga, mizozo na vita vinazidi kuongeza ukatili dhidi ya wanawake na wasichana na kuchochea visababishi na hatari zaidi vya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.

Hapa nchini, inaelezwa kuwa asilimia 40 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili au kingono mara moja au zaidi katika kipindi cha maisha yao.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anasema taarifa za Utafiti wa Afya ya Uzazi na Viashiria vya Malaria inaonesha pia kwa mwaka 2015/16 asilimia 20 ya wanawake wa umri huo wameingiliwa kimwili bila ridhaa yao.

Kwa hali kama hiyo, ninadhani kuna haja ya kuwa na mikakati madhubuti ya kudhibiti vitendo vyote vya ukatili ili kuwalinda wanawake na wasichana ambao wanatajwa kuwa waathirika wakubwa.

Wizara inasema kuna Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Tanzania (MTAKUWWA) unaolenga kuongeza msaada wa kielimu ili kuwajengea waathirika uelewa.

Hilo ni jambo jema, kwani mtu akiwa na uelewa wa kutosha kuhusu haki yake, inaweza kuwa rahisi kwake kutoa taarifa anapoona viashiria vya ukatili au anapofanyiwa vitendo vya ukatili.

Katika maeneo mbalimbali, kuna kamati za ulinzi wa wanawake na watoto 1,8126 ngazi ya taifa, mkoa, halmashauri, kata, vijiji na mitaa. Kwa kutumia nyenzo hizo, inaweza kuwa rahisi kudhibiti ukatili.

Serikali ina wajibu wa kuandaa mikakati madhubuti iliyoboreshwa itakayosaidia kuimarisha Kamati za MTAKUWWA ikiwamo kutenga bajeti kwa kushirikiana na wadau, ili kutekeleza mpango kazi huo.

Pia, jamii iwe tayari kushirikiana na serikali kwa kutoa taarifa zitakazosaidia kuwabana wale wote wanaoshiriki vitendo vya ukatili hata kama watuhumiwa watakuwa ni ndugu. Wapo baadhi ya watu ambao huwaficha watuhumiwa hasa wale wanaobainika kuwa wahusika ni ndugu au kumalizana na wale wanaofanya vitendo hivyo kwa kulipwa fedha.

Ni aibu, mtu anabaka au analawiti, halafu anafichwa eti kwa sababu ni ndugu au anatoa fedha ili kumalizana na wazazi ama familia, kitendo ambacho kinaweza kusababisha ukatili kuendelea ndani ya jamii.

Wataalam wa saikolojia wanasema, ukatili unaweza kuwa ukatili wa kingono, unaoweza kusababisha magonjwa kama UKIMWI, lakini pia kuna ukatili wa vipigo na kwamba suala la athari kisaikolojia zinaweza kufanana.

Mojawapo ya athari zinazotajwa na wataalam hao ni kutojiamini, kutoamini watu, kutojikubali na kwamba mazingira kama hayo, wanatakiwa kukutana na watu wa saikolojia ili kuzungumza nao, kuwashauri ili kuwaweka sawa.

Wanasema ukatili wa kijinsia una madhara mengi, na kwamba matokeo yake ni mabaya kwa wanawake na watoto, kwa kuwa yanaweza kudumu katika kipindi chote cha maisha ya 'manusura' kama hawakupata wataalam wa saikolojia kwa ajili ya kuwaweka sawa.

Aidha, wanaweka wazi kuwa, ukatili huo unaweza kuharibu fursa ya mtu kuishi maisha mazuri, yenye afya na mafanikio na yanaweza kuathiri mtu kiafya, kimwili, kisaikolojia na kiroho, kuathiri uwezo wa mwanamke kushiriki katika masuala ya kiuchumi na kufifisha uwezo wake katika kuboresha maisha ya familia.

Kimsingi, ukatili huo haupaswi kuwa sehemu ya maisha ya kila siku kwa wanawake na wasichana wa Kitanzania kwani kama wanavyosema wataalam wa saikolojia, una madhara makubwa katika maisha.

Mikakati zaidi ni muhimu kwa ajili ya kukomesha ukatili kwa wanawake na wasichana ili waweze kuishi kwa amani katika nchi yao. Jambo la msingi ni kila mmoja kushiriki katika vita dhidi ya vitendo hivyo.

# Mwinyi aihakikishia Uingereza kudhibiti trachoma Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameihakikishia Uingereza kwamba Zanzibar inaendelea na mikakati na juhudi za kudhibiti na kuumaliza ugonjwa wa "trachoma" nchini.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Princess Sophie (Duchess of Edinburgh) aliyepo Zanzibar kwa ziara ya siku sita Tanzania kutembelea miradi mbalimbali ya afya inayotekelezwa na taasisi tofauti ambazo yeye ni mlezi.

Rais Dk. Mwinyi alisema hatua iliyofikiwa na Zanzibar ya kukabiliana na magonjwa mbalimbali inatokana na juhudi kubwa na misaada ya afya inayotolewa na Uingereza na kumwahidi kuwa Zanzibar itaendelea kufanyakazi kwa juhudi zaidi ili kupambana na magonjwa hasa yasiyoambukiza (NCDs) yanayoathiri ustawi wa jamii.

Pia, Rais Dk. Mwinyi alieleza kufarajika kwake kwa misaada ya mafunzo ya kitaalamu ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Sekta ya Afya hasa katika kukabiliana na

maradhi yasiyoambukiza yanayotolewa na nchi hiyo ambayo yamekuwa kichocheo muhimu cha kuleta mafanikio kwenye Sekta ya Afya na kusisitiza misaada hiyo kuendelezwa.

Dk. Mwinyi alimhakikishia Princess Sophie kuwa Zanzibar inaendelea kuweka mkazo zaidi na kuhakikisha huduma bora za afya hususan kuimarisha huduma za kitengo cha uzazi kwa mama na mtoto na kuwataka wafadhili na washirika wengine wa maendeleo kuendelea kuiunga mkono Zanzibar.

Naye, Princess Sophie ameipongeza Zanzibar kwa hatua iliyofikia katika kuudhibiti ugonjwa wa 'trachoma' kwa kiasi kikubwa na kufikia mapema malengo yaliyowekwa na Jumuiya ya Madola (Commonwealth) ya kumaliza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

Alisema, Zanzibar ni miongoni mwa nchi za mfano zilizofanikiwa kuudhibiti na kuutokomeza ugonjwa huo ambao umekuwa tishio kwa nchi nyingi barani Afrika pia aliisisitiza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa ugonjwa huo haujirudii.

Alisema ameridhishwa na maendeleo ya miradi inayoungwa mkono na nchi yake kwenye Sekta ya Afya na kumhakikisha Rais Mwinyi kwa taasisi zote zinazoendesha miradi hiyo, kuendelea na misaada yake.

Princess Sophie (Duchess of Edinburgh) ni mke wa mtoto wa mwisho wa aliyekua Malkia wa Uingereza, Elizabeth II, Prince Edward ambaye ni mdogo wa Mfalme wa sasa wa Uingeza, Charles III.



Baadhi ya wamiliki wa kampuni za mabasi yanayotoa huduma za usafiri saa 24, wakifuatilia semina kuhusu Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na matumizi sahihi ya kitufe cha utambuzi wa dereva (I-Button), iliyoendeshwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mzazi wa mwanafunzi aliyetoweka amtaka akiwa hai

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

KUTOWEKA katika mazingira ya kutatanisha kwa mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Bagara iliyoko Babati mkoani Manyara, Joel Johannes (14), katika Mlima Kwaraa wakati wa ziara ya mafunzo, kumeleta taharuki kwa familia yake, huku ikitoa masharti ya mtoto wao kupatikana akiwa hai.

Joel, aliyetoweka Septemba 13, mwaka huu, alikuwa ni miongoni mwa wanafunzi 103 wa shule hiyo waliokuwa wamegawanywa makundi matatu katika safari ya kimasomo.

Inaelezwa kuwa wakati wa kurudi, wanafunzi hao baadhi yao akiwamo Joel walidaiwa kupotea njia, lakini wenzake walipatikana isipokuwa yeye.

Akizungumzia mkasa huo, Johannes Mariki, ambaye ni baba wa mwanafunzi huyo, alisema; "Anayehitajika awajibike ni uongozi wa shule. Ninamtaka mtoto wangu akiwa hai, sio kwamba tunashindwa kukaa naye nyumbani, tumewaletea watoto wetu muwatunze hatudaiwi chochote."

"Unaniambia mnampeleka safari halafu haonekani, hapana haiwezekani. Hata jana mbele ya Ofisa wa Upelelezi (Mkuu wa Upelezi wa Wilaya-OC CID), nimewaambia nahitaji mtoto wangu akiwa hai, kama hawana ulinzi, kwa nini walienda kujifunza huko mlimani?

Alisema Septemba 13, siku ya safari hiyo alipigiwa simu kuwa mtoto wake haonekani na kutokana na tukio hilo, familia yake imelazimika kuwasiliana na baadhi ya ndugu ili kuongeza kumtafuta ndugu yao.

"Tulikuja tukaungana nao, tukaondoka hadi mahali wanaita 'Chokaa' ni mbali sana, ila tulivyofika pale tukakuta zimamoto wanarudi kutoka mlimani, wakasema wamemtafuta kule hawajamuona, nasi tukarudi pale," alisema baba mzazi wa mwanafunzi huyo.

Kwa mujibu wa mzazi huyo, kuna kijana alisema kuna mama alikuwa anaokota kuni, alidai kumuona kijana akishuka mlimani mwenyewe akiwa amevalia sare za shule na alipooneshwa picha alikiri kuwa ni yeye.

"Jumatatu sisi tulikuja shuleni, tukaingia hamna mwalimu, nikampigia mkuu wa shule, kuuliza kuhusu hili suala. Nikamwambia kama hamna ushirikiano tunaenda kwa Mkuu wa mkoa au Mkuu wa wilaya; Na tulivyofika pale tukamkuta Katibu Tawala wa Wilaya, ambaye aliwaita na tukatoa maelezo," alisema.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Makarani Ahmed, alisema hadi sasa jeshi hilo linaendelea na uchunguzi, ikiwamo operesheni ya kumsaka Joel aliko, huku akieleza kwa siku nne mfululizo hawajafanikiwa kumuona akiwa hai au kuuona mwili wake.

MZAZI ALISITA

Baba mzazi wa Johannes, alisema alisita kuhusu safari hiyo, akidai wiki mbili zilizopita baada ya kujulishwa na uongozi wa shule hiyo, alikataa mtoto wake kwenda kwenye ziara ya mafunzo, lakini baadaye alilazimika kumruhusu kwa kuwa ni mtoto wa pekee wa kiume na alikuwa akilalamika kuwa ni yeye pekee ndiye hajalipa kwenda safari hiyo.

"Tuko siku ya nne leo hii hapa, hawajui gharama tunazotumia tumeacha shughuli zetu tunamtaka Joel wetu kwanza, yaani ninamhitaji Joel akiwa mzima na afya yake," alisisitiza mzazi huyo.

Mama wa mtoto huyo, Germana Wilbard, alidai kupigiwa simu na mmoja wa walimu, akimwomba namba za shangazi wa Joel anayeishi Babati na alipouliza kuna shida gani alijibiwa hakuna; lakini baada ya shangazi huyo kutokupokea, walijulishwa mtoto wao amepotea.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Simon Mumbee, alisema katika safari hiyo wanafunzi 103 walienda wakiwa na walimu wao na waongozaji.

Alisema baada ya kubainika Joel kutokuwapo, waongoza mlima hao walirudi mlimani kufuatilia na hadi saa sita usiku walikuwa mlimani huko bila mafaniko yoyote.

Alisema jitihada mbalimbali zinaendelea zikiongozwa na Jeshi la Polisi, halmashauri hiyo na kuwa wamelazimika kushirkisha jamii ya pembezoni mwa mlima huo.

Mumbee, alisema imeundwa timu akiwamo Ofisa Elimu Sekondari, ambayo imeenda shuleni kuzungumza na marafiki zake Joel ili kupata taarifa zaidi.

"Pia tumeagiza jeshi la akiba pia linaenda ili kuungana na waliopo kule kufanya operesheni hiyo kumtafuta," alisema Mumbee.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

# Waandishi IPP Media wapenya orodha ya wateule tuzo za EJAT

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT) limetangaza majina 72 ya wateule wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2023, huku kampuni za IPP Media zikiwa na wateule saba.

Waandishi wa IPP walioteuliwa na jopo la majaji kuingia katika kinyang'anyiro hicho kwa gazeti Nipashe ni Sanula Athanas (Dar), Abdallah Nassoro (Mtwara), Marco Maduhu (Shinyanga), Halfani Chusi (Dar) na Christina Mwakangale (Dar).

Wengine ni Rodgers Simon na Benjamin Mzinga, wote ITV mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kutangaza wateule hao jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT 2023, Ernest Sungura, alisema washindi wa vipengele 20 vinavyoshindaniwa, mshindi wa jumla na wa mafanikio ya maisha katika uandishi wa habari (LAJA) watajulikana Septemba 28 mwaka huu.

Mgeni rasmi katika tuzo hizo ambazo zinatolewa kwa mara ya 15 mfululizo anatarajiwa kuwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Alisema kuwa kati ya waandishi 72 walioteuliwa kuingia katika kinyang'anyiro cha kushindania tuzo hizo, wanaume ni 45 na wanawake ni 27.

Wateule wanaotoka kwenye magazeti ni 25, luninga 14, vyombo vya mtandaoni ni 13 na redio zina wateule 20.

Sungura alisema kazi za zilizowasilishwa kwa ajili ya EJAT 2023 zimeongezeka hadi kufikia 1,135 kutoka kazi 893 za mwaka 2022, kazi 606 mwaka 2021 na 396 za mwaka 2020.

Alisema waandishi wa mkoa wa Dar es Salaam mwaka huu wameongoza, wakiwasilisha kazi 290, wakifuatiwa na mkoa wa Aruska kazi 81, Mwanza 74, Iringa 72 na Mtwara 49.

Kwa upande wa Zanzibar, kazi zilizowasilishwa ni kutoka Kaskazini Pemba (36), Pemba Kusini (43), na Mjini Magharibi (29).

Sungura alisema moja ya mambo la kipekee katika kilele cha tuzo hizo mwaka huu ni kusikia kutoka kwa majaji kuhusu viwango vya uandishi wa habari za magazeti, redio, televisheni na mitandaoni juu ya habari zilizohusu uwekezaji wa kampuni ya DP World katika Bandari za Tanzania, hali ya Ngorongoro na jamii ya Maasai inayoishi huko pamoja na maporomoko ya Hanang'.

Sungura alisema siku hiyo ya kilele cha tuzo, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, atazindua Jarida la Tuzo pamoja na Tuzo za Magazine, matukio yote mawili yakitajwa yatahamasisha umahiri katika sekta mbalimbali Tanzania na nje.

"Kwa kuanzia, majarida hayo, moja la Kiswahili na lingine la Kiingereza yatabeba maudhui ya tuzo za umahiri wa uandishi wa habari wa Tanzania.

"Moja ya maudhui katika majarida yote mawili ni simulizi ya maisha ya wateule wote, na kazi ya kuandika simulizi hizo inaanza leo (jana). Hivyo, wateule wote wawe tayari kufikiwa na waandishi wa jarida hilo kuanzia sasa.

"Maudhui mengine yatahusu wafadhili wa tuzo juu ya mchango wao katika kubadilisha maisha ya watu, ikiwamo kukuza na kujenga tasnia ya habari," Sungura alisema.

Jopo la majaji waliofanya kazi ya kupitia kazi hizo zilizowasilisha na waandishi wa habari liliongozwa na Mwenyekiti Halima Shariff, Katibu akiwa Dk. Egbert Mkoko kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Majaji wengine ni Mkumbwa Ally, Eshe Muhiddin, Jeniffer Sumi, Halima Msellemu na Absalom Kibanda.



Daraja la mto Pangani lenye urefu wa mita 525 na barabara unganishi (Km 14.3), mkoani Tanga zikiendelea kujengwa. Daraja hili linajengwa na mkandarasi Shandong Luqiao Group. **PICHA: WIZARA YA UJENZI**

## Wajipanga kuendesha baiskeli hadi Butiama kumuenzi Nyerere

**Na Halfani Chusi**

KATIKA kuenzi mema aliyofanya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kampuni ya simu za mkononi Vodacom Tanzania na Benki ya Stanbic zimetangaza msafara wa baiskeli mpaka Butiama.

Msafara huo una lengo la kusaidia uboreshwaji huduma za afya, elimu, utunzaji mazingira, kuongeza uelewa wa kusoma na kuandika pamoja na kutoa ujuzi maalumu wa kuwawezesha wananchi kufanikiwa kiuchumi.

Hayo yalisemwa juzi mkoani Dar es Salaam na Mkuu wa Uhusiano ya Vyombo vya Habari wa Vodacom Tanzania, Annette Kanora.

"Kupitia ushirikiano huu, tutaweka msisitizo juu ya uhifadhi wa mazingira na huduma za afya na maendeleo ya jamii kiujumla kuendana na maadili yaliyohimizwa na Mwalimu Nyerere.

"Ziara hii itajumuisha shughuli mbalimbali, zikiwamo warsha za elimu, kambi za afya na kampeni za kuhamasisha uelewa wa mazingira, zikifikia jamii kote Tanzania.

"Ushirikiano huu unaonesha kujitolea kwetu kwa pamoja katika kuleta athari chanya za kijamii kote nchini. Kwa kuunganisha nguvu zetu, tunaweza kuendeleza maono ya Nyerere ya taifa lenye ustawi na ushirikishwaji," alisema Annette.

Meneja Uhusiano na Chapa wa Stanbic Bank Tanzania, Annette Nkini, alisema, "Kuwekeza katika elimu, afya na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni sehemu kuu ya uwekezaji wetu wa kijamii na juhudi endelevu. Tunafurahi kushirikiana na Vodacom kuleta athari chanya kwenye jamii."

Ziara hiyo itaanza rasmi Septemba 29 na itawakutanisha waendesha baiskeli ndani na nje ya nchi.

# Waziri: Tutumie nishati safi kuepuka uharibifu wa misitu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Maliasili na utalii, Dunstan Kitandula amewaomba wadau wa misitu nchini kuweka msisitizo kwa jamii kujikita katika matumizi ya nishati safi.

Alitoa rai hiyo jana wakati wa Mkutano Mkuu wa 24 wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), akiwakilisha Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana mjini hapa.

Alisema serikali inahakikisha watu wanaachana na kutumia nishati zisizo salama na kutumia nishati safi, akisisitiza "ni jambo lililovaliwa njuga hadi kufikia nchi kupongezwa na kupewa jukumu la kuongoza suala hilo kimataifa."

Alisema nishati safi ni jitihada za kuondokana na matumizi holela ya uchomaji mkaa na kukata miti ovyo, shughuli zinazofanywa ili kutengeneza mkaa unaotumiwa majumbani na kwamba mbadala wa mkaa unapaswa kuwa nishati safi, yakiwamo mabaki ya miti na pumba.

"Utengenezaji mkaa mbadala unasaidia kuhakikisha hewa chafu inaondolewa kwenye mkaa huo na kufanya mkaa huu kuwa salama kuliko ule mwingine, ninaunga mkono jitihada zinazofanywa na sekta binafsi, taasisi za kiserikali kwa kuhakikisha tunaachana na matumizi ya mkaa unaoharibu mazingira na kuja na teknolojia mpya, ukiwamo utengenezaji mkaa wa mabaki ya makaa ya mawe, pumba na mabaki ya miti, huku tukisisitiza matumizi ya gesi na umeme kuepuka uharibifu wa mazingira," alisema

Kitandula alisema nchi inapita kipindi kigumu kutokana na uharibifu wa mazingira kuwa mkubwa, ukichangia upotevu misitu kwa hekta 469,000 kila mwaka.

Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, Emmanuel Msofe alitaka jamii kutekeleza mikakati iliyowekwa ili kuhakikisha uharibifu wa misitu hauendelei.

Alitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kilimo misitu kinachosaidia kuchanganya mazao ya chakula na misitu ili kuendeleza rasilimali za misitu na mkakati wa mianzi unaohamasisha jamii kupanda mianzi ili kupata bidhaa na huduma mbalimbali zinazotokana na bidhaa za mianzi kwa ajili ya matumizi na kupunguza athari za upotevu wa misitu nchini.

Mkurugenzi wa MJUMITA, Rahima Njaidi aliwahimiza wadau wa misitu kutumia misitu kwa njia endelevu ili iwasaidie kuongeza kipato na kuboresha maisha.

Alisema MJUMITA ina mikakati ya kukabiliana na matumizi ya nishati chafu kwa kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi ya nishati mbadala,



# Wanaohama Ngorongoro wapewa mahindi kila kaya

**Na Godfrey Mushi,**
HANDENI

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imeongeza motisha kwa wafugaji wa jamii ya kimasai wanaohama kwa hiari ndani ya eneo la hifadhi hiyo kwenda Msomera Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, kwa kugawa mahindi ya chakula kwa kila kaya. Wananchi hao wanapatiwa mahindi gunia 12 kila kaya, kwa muda wa miezi 18 ya mwanzo.

Jana, Kamishina Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, anayesimamia Idara ya Maendeleo ya Jamii ya NCAA, Gloria Bideberi akiongoza zoezi la ugawaji wa mahindi hayo, alisema utaratibu huo ni endelevu kwa kila baada ya miezi mitatu.

"Serikali kupitia NCAA, imeendelea kutimiza ahadi ya kugawa chakula kwa wananchi waliotoka eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kuhamia Kijiji cha Msomera. Tunawapa gunia mbili za mahindi kila kaya, ambapo mpango huo hufanyika kila baada ya miezi mitatu kwa kipindi cha miezi 18, wakiwa wanaendelea kuzoea mazingira," alisema.

**"Serikali kupitia NCAA, imeendelea kutimiza ahadi ya kugawa chakula kwa wananchi waliotoka eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kuhamia Kijiji cha Msomera...."**

Hadi kufikia Septemba 18 mwaka huu, kaya 1,451 zimenufaika na mgawo wa mahindi wa tani 945 kwa awamu tofauti.

Kabla ya ugawaji wa huo, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Abert Msando, alisema zoezi la ugawaji wa mahindi kwa wananchi hao ni mpango wa serikali wa kuhakikisha kuwa wanachi wote wanaohamia Msomera wanapatiwa maisha bora zaidi tofauti na walikotoka.

Alisema mpango huo ni mahususi kwa sababu sheria za uhifadhi ziliwabana kufanya baadhi ya shughuli kama kilimo. Baada ya kukamilika zoezi hilo, Sabore Olemoko, ambaye ni mmoja kati ya wananchi wanaonufaika na mpango huo, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwajali na kubainisha kuwa wanafurahia maisha wanayoishi Msomera hasa kukuta huduma zote muhimu za kijamii na



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah (wapili kushoto) akikabidhi zawadi ya vifaa vya elimu kwa wanafunzi katika utambulisho wa kampeni ya "Mtoto wa Leo, Samia wa kesho" katika Shule ya Sekondari Kwabastola kata ya Makole, ambapo pia alitembelea Shule ya Msingi Makole, Shule ya Msingi Pangamlima na kugawa vifaa vya shule na pedi. Kushoto ni diwani wa kata ya Makole, Shabani Achimwene na kulia Mkuu wa Shule ya Sekondari Kwabastola, Juma Rashid Mdachi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Msuya amdokeza Askofu Malasusa mrithi wa Dk. Sendoro

**Na Mary Mosha,** MWANGA

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Cleopa Msuya, amemdokeza Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa kwamba wananchi wa Mwanga, wanamhitaji Askofu mpya anayeweza kutafsiri, kuyaishi maono na matendo yake kwa vitendo.

Amesema wakati ukifika wa kutafuta mrithi wa kiti cha Askofu wa Dayosisi ya Mwanga ya KKKT, kanisa lisisite kuwapatia mtu anayeweza kuwaunganisha wana Mwanga, atakayevaa viatu vya Askofu wa Dayosisi hiyo, marehemu Dk. Chediel Sendoro.

Msuya alikuwa akimzungumzia marehemu Dk. Chediel Sendoro aliyefariki dunia Septemba 9 mwaka huu kwa ajali ya gari, majira ya saa 1:30 usiku; baada ya gari alilokuwa akiliendesha aina ya Toyota Prado, kugongana na lori aina ya scania katika eneo la Kisangiro wilayani Mwanga.

Dk. Chediel Sendoro, ni mtoto wa Askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Elinaza Sendoro.

Msuya alisema: "Sasa viongozi wa KKKT, mjipange kuhakikisha kwamba mnampata kiongozi atakayeweza kuendeleza kazi aliyoianzisha Askofu Dk. Chidiel. Mara nyingi kazi hiyo huonekana ni nyeupe, ila ni ngumu kupata mtu mwenye ari ya kuujenga umoja na upendo".

Askofu Sendoro, ambaye hadi anafariki dunia alikuwa mhitimu wa Shahada ya Uzamivu (PhD) na Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA); alizaliwa Mei 1, 1970 akiwa mtoto wa nne wa Askofu Dk. Elinaza Sendoro.

Mbunge wa Mwanga, Joseph Tadayo, amemtaja Dk. Chediel Sendoro kama kiongozi wa imani aliyependa kuwa msuluhishi katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Mwanga.

# Serikali yaagiza kuimarishwa ulinzi mipakani

**Na Cynthia Mwilolezi,**
LONGIDO

SERIKALI imeagiza maeneo yote ya mipakani ulinzi uimarishwe ili kuhakikikisha hakuna matukio yanayoharibu taswira ya nchi, huku ikielekeza ngazi za mikoa kupima kila mgeni anayeingia nchini ili kudhibiti ugonjwa wa homa ya nyani.

Agizo hilo limetolewa jana wilayani Longido mkoani Arusha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa.

Pamoja na mambo mengine aliagiza maeneo yote ya mipaka ulinzi wake uimarishwe, ili kuhakikikisha hakuna matukio yanayoharibu taswira ya nchi.

Alisema kuna baadhi ya watu wanahujumu nchi kwa kuingiza magendo hususani maeneo ya mipakani, hivyo alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda kwa kugawa mafuta lita zaidi ya 25,000 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi, ikiwemo kutoa mafuta kwa vyombo vya ulinzi na usalama.

"Huu ni ubunifu unaotakiwa kwa ajili ya kuhakikikisha ulinzi na usalama unaimarishwa. Hakikisheni mipaka yetu hasa ya mpaka wa Kituo cha Forodha cha Pamoja (OSBP) cha Namanga, kinakuwa salama lakini pia tambueni kuwa kuna changamoto ya ugonjwa wa homa ya nyani ambao upo nchi jirani, hivyo imarisheni usalama maeneo ya mipakani,"alisema.

Alisema ugonjwa huo haupo mbali, hivyo msingi wa kuimarisha mipaka hiyo utatusaidia kudhibiti ugonjwa huo kwa kushirkiana na Wizara ya Afya.

Vilevile aliagiza kukaguliwa kwa wageni wanaoingia nchini kwenye maeneo ya mipakani, ili kudhibiti ugonjwa huo na taratibu nyingine za kiafya zichukuliwe, ikiwemo kudhibiti magendo yanayoingia mipakani yajulikane.

Kuhusu changamoto ya skana alisema ataongea na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba kwa ajili ya kuhakikikisha inafika mpakani Namanga.

Pia, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Longido, Salum Kalli, kuhakikikisha anashirikiana na watumishi, chama na viongozi katika kuwaleta maendeleo wananchi.

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikikisha ndoto zao na changamoto zinazowakabili zinatatuliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alisema mkoa huo umejipanga kuhakikikisha unatatua chagamoto ya maji kwa wananchi kwa kutengewa maeneo ya mifugo kunywa maji.

Alisema kwa kuanzia Wilaya ya Ngorongoro umeanza utekelezaji huo kwa kuchimba visima 17 kutengewa maeneo ya mifugo kunywa maji na kuondoa changamoto kati ya wafugaji na wakulima.

Pia alisema mkoa huo sasa upo katika hatua ya tatu ya kulima kilimo cha nyasi, ili kuondoa changamoto ya mifugo kukosa chakula na kutembea umbali mrefu kupata malisho.

"Lengo letu tuondokane na migogoro baina ya wafugaji na wakulima ikiwemo upatikanaji wa maji kwa mifugo yao kwani kwa mkoa huu mifugo ni siasa, hivyo tumekuwa na awamu ya tatu ya ulimaji wa kilimo wa nyasi,"alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Salum Kalli, alisema wilaya hiyo iliyopo mpakani wa Tanzania na Kenya imejipanga kukabiliana na ugonjwa wa homa ya nyani.

Alisema pia wanajiandaa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ikiwemo kuhakikisha inatatua changamoto ya wananchi kukata mabomba ya maji.







Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi akizungumza katika mkutano wa kusikiliza kero za wananchi alipokuwa kijiji cha Kigera Etuma wilaya ya Musoma jana. Kushoto ni mkuu wa wilaya hiyo Juma Chikoka na kulia ni Mwenyekiti wa kijiji hicho Magafu Kitundure. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Abiria wadaiwa kuwashambulia 'trafiki' wawili wakikagua gari

**Na Vitus Audax**

BAADHI ya abiria, kondakta pamoja na utingo waliokuwa katika gari la abiria namba T476 ECP aina ya TATA lililokuwa likitokea mkoani Mwanza kwenda Serengeti wanatuhumiwa kuwashambulia askari wawili wa usalama barabarani walioingia ndani ya gari hio kwa ajili ya kufanya ukaguzi.

Katika tukio hilo lililotokea juzi majira ya saa sita mchana katika maeneo ya Kijiji cha Natta, Barabara ya Bunda-Mgumu ambako inadaiwa kuwa baada ya askari hao kuingia ndani ya gari dereva alianza kuendeha kisha kuanza kushambuliwa.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, ACP Menrad Sindano alitaja askari waliojeruhiwa kuwa ni pamoja na Koplo Peter pamoja na Koplo Paulo ambaye alijeruhiwa jicho la kulia.

"Askari hao wakiwa katika majukumu yao ya kikazi walisimamisha gari hilo mali ya Kampuni ya Jimmy Safari ambalo lilikuwa likiendeshwa na January Ally baada ya kusimama walianza ukaguzi wa gali hilo lililokuwa limezidisha abiria," alisema.

Aliongeza: "Waliingia ndani kwaajili ya ukaguzi zaidi lakini dereva aliondoa gari hilo, huku kondakta, utingo na baadhi ya abiria wakaanza kuwashambulia askari hao kwa kuwapiga sehemu mbalimbali za mwili".

Aidha alisema polisi inawashikilia watuhumiwa 15 kwa ajili ya upelelezi zaidi kuhusiana na tukio hilo na baada ya upelelezi kukamilika jalada litapelekwa ofisi ya mwendesha mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

# RC atoa maagizo RUWASA upangaji bei za maji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda ameuagiza Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) mkoani hapa kuwashirikisha wananchi kupitia vikao ili kupata bei za maji zilizo rafiki.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akikagua ukarabati wa mradi wa maji uliotekelezwa na serikali kupitia mradi wa Uviko -19 katika Kijiji cha Kahangara wilayani Magu kwa Sh.milioni 508.

Aidha aliutaka wakala huo kupitia wasimamizi wa Jumuiya za Watumia Maji (CBWSO) kutokupandisha bei za maji kiholela kwani kwa kufanya hivyo ni kuwagombanisha wananchi na serikali.

Hivyo aliwataka kuendelea kutoza bei ambazo ziliamuliwa na mikutano ya kijiji tu na siyo vinginevyo.

Mtanda alisema: "Serikali inatekeleza miradi ya huduma za jamii hususani maji kama unavyotarajiwa kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kutoka asilimia 34 hadi 90, hivyo watendaji ni lazima wasimamie ukamilifu wa hilo".

Aidha, aliwataka RUWASA kuhakikisha kuwa kupitia mradi huo wanafikisha huduma za maji kwenye vijiji vyote ambavyo bado havijapata maji safi na salama ndani ya kata hiyo na kusimamia miundombinu hiyo ili maji yaendelee kutoka kila siku.

Meneja RUWASA Wilaya ya Magu, Daud Amlima alisema mradi huo umeshakamilisha vitua 34 vya kuchotea maji ambayo vinatoa maji na kwamba unasimamiwa na wananchi wenyewe kupitia jumuia zao.

# Wananchi wang'aka kutosomewa mapato na matumizi

**Na Samson Chacha,** TARIME

BAADHI ya wananchi katika Halmashauri ya Tarime Vijijini mkoani Mara wamewataka viongozi wa halmashauri hiyo kuweka utaratibu maalum kwa wenyeviti wa vijiji, mitaa na watendaji kata kuwasomea mapato na matumizi.

Wananchi hao kutoka kata tatu kati ya 26 za Sirari, Matongo na Kemambo zilizopo katika halmashauri hiyo zinazotajwa kuwa na vyanzo vingi vya mapato vikiwemo viwanda vya kukoboa mchele zaidi ya 10.

Pia ina viwanda vya alizeti 2 vituo vya mafuta zaidi ya vitano, wachimbaji wadogo wa madini zaidi ya 100, kampuni za uchimbaji madini ukiwemo mgodi wa North Mara.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti akiwemo Julius Makima, alisema kutokusomewa mapato na matumizi kumekuwa kukiwatia hofu juu ya fedha za umma zinavyotumika, huku baadhi ya miradi ya kimkakati ikiendelea kukwama.

Makima alitaja miradi iliyokwama ni pamoja na Soko la Kimataifa Remagwe, Stendi ya Mabasi Ngerengere pamoja na upungufu wa madawati katika baadhi ya shule.

Naye Nyangoko Paulo alisema licha ya makusanyo makubwa ya fedha katika soko, stendi ya mabasi na daladala pamoja vizuizi vya TRA bado wamejaribu kuwahimiza wenyeviti wa vijiji waitishe mikutano na kuwasomea mapato na matumizi lakini hawafanyi hivyo.

"Licha ya kuwa na vyanzo vingi vya mapato, watu hawana maji greda la kukarabati barabara walilosema kununua hatulioni na taarifa hatupewi," alisema Mwita Nyamhanga.

Diwani wa Kata ya Sirari, Amos Sagara alikiri kuwepo kwa miradi ya kimkakati iliyopangwa kutekelezwa lakini baadhi imekwama ukiwemo ujenzi wa Soko la Kimataifa Remagwe mbali na kujengwa misingi na kutumika kwa zaidi ya Sh.bilioni moja.

Kadhalika alisema mradi mwingine ni Stendi ya Mabasi ya Ng'ereng'ere ambayo ilijengwa vibanda vinne, choo na kibanda cha wasafiri na mabasi hayaingii katika stendi hiyo mbali ya kuwepo mkata ushuru.

Alisema kumekuwa na ahadi za mara kwa mara, kwamba hata madiwani wanatamani miradi ya mikakati ikamilike ianze kutoa huduma kwa wananchi.

Kuhusu ununuzi wa greda, Diwani wa Kata ya Mbogi, Nyahiri Magarya alikiri kutengwa kwa zaidi ya Sh.milioni 800 kwa ajili ya ununuzi wa gari hilo lakini zilibadilishiwa matumizi na kupelekwa katika kila kata kupewa Sh. milioni 20 kwa ajili ya ukarabati wa barabara zilizoharibika wakati wa mvua za El-nino.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Tarime Vijijini, Solomon Shati alipoulizwa na Nipashe kuhusu fedha zianzokusanya na halmashauri yake pamoja na matumizi yake kutosomwa katika mikutano ya vijiji ambapo wananchi wanauliza alisema jukumu hilo ni la wenyeviti wa vijiji na watendaji.

Alisema: "Kuhusu kununua greda na kukwama miradi ya Soko la Remagwe na Stendi ya Ng'ereng'ere tunagemea kupata fedha kutoka serikalini ili kukamilisha miradi hiyo ili iweze kutoa huduma kwa wananchi kwa sababu hata sisi hatutamani miradi hiyo ikwame".




Ukurasa 13

Hii miti inavyokatwa ovyo, tutalia na kusaga meno huko tunakong'ang'ania



**Chereko Rufiji, mbaazi sasa zao la mnada, bei yaruka 300/- hadi 1,753.**

Ukurasa 12

BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 20, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Jafo na mchakamchaka wa maagizo 2 ya Rais kazini Viwanda, Biashara

## • Siku 24 baada kiapo atua 'Kariakoo ya kimataifa'

**Na Mwandishi Wetu**

ILIKUWA mwezi Julai mwaka huu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipomuapisha Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo na wenzake, akimuagiza "asiwe mtu wa kukaa ofisini pekee, bali kufika kwa wananchi kukagua kinachoendelea."

"Nianze na Jafo, ulikuwa Ofisi ya Makamu wa Rais umefanya vizuri! Lakini, nimeona nikutoe nikupeleke biashara kwa sababu biashara pilika ni nyingi mno na kuanzia sasa pale ofisini mwenzio alipokuwa anakaa sitaki ukae.

"Namuelewa Waziri kwanini alikuwa haendi huko kwa kazi ninayotaka kukupa, kwa mtoto wa kike sio rahisi, kushinda Kariakoo juu chini, chini juu sio rahisi, hiyo kazi nataka uifanye wewe."

Akaendelea: "Kariakoo ni eneo zuri sana la biashara na eneo muhimu sana la biashara na ndio linalofanya Dar es salaam iitwe 'kitovu cha biashara', kwa sababu mataifa yote yanakuja Kariakoo.

"Lakini, Kariakoo tumeweka pesa nyingi sana kujenga yale masoko ya Kariakoo na masoko yakimalizika nataka biashara zifanyike saa 24 kwa hiyo, mtakaa vipi na Jeshi la Polisi mtajipanga vipi, hiyo ni kazi yako.

"Nataka Kariakoo pawe na Soko la Biashara la Kimataifa na kwa sababu mwaka huu 'mwisho mwisho' tunamaliza yale majengo, Wamachinga na wengine walioko pale wataingizwa ndani ya soko."

Hadi sasa, baadhi ya wafanyabiashara wa kigeni Waafrika wanaopatikana Kariakoo kufuata bidhaa ni kutoka nchi kama Malawi, Zimbabwe na Zambia, huku kukiwapo uwekezaji biashara kimataifa kutoka wageni wa nchi kama China.



Siku Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipotembelea Soko la Kariakoo, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

Pia, Rais Dk. Samia akaisisitiza hoja yake aliyotoa siku chache kabla ya tukio hilo, akitamka: "Pia ukarejee Ilani yetu ya Uchaguzi inayozungumzia Sekta ya Biashara na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua.

"Ukarejee kauli yangu kwenye ufunguzi wa maonyesho ya Sabasaba nimesema, serikali itafanya kila linalowezekana kusikiliza na kutatua changamoto za wafanyabiashara nchini na ndio maana nakuambia uwe juu chini Kariakoo"

Baada ya uteuzi, uliobeba magizio makuu mawili, uihuishaji wa biashara Karikaoo na kufanya biashra ya ushindani kitaifa, siku iliyofuata Julai 6, Waziri Jafo akaanza kazi ya ukaguzi na kushughulilikia agizo la Rais, hatua yake ya kwanza ni sokoni Kariakoo.

Hapo azma kubwa ilikuwa kupata undani wa shida zao na akakutana na viongozi wa wafanyabiashara waliomjibu kuona dalili za afueni.

### AKIWAJIBIKIA MAELEKEZO

Ndio imekuwa staili ya kazi, akizuru na kukagua maeneio ya kazi, huku akisafiri na ajenda mbili za rais.

Waziri Dk. Jafo akiwa bungeni mwezi uliopita, akabainisha hatua za serikali katika kusimamia ushindani wa haki na kuwalinda watumiaji bidhaa na huduma nchini, kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003, inayotarajiwa kufanyiwa marekebisho karibuni ya tija kumlinda mlaji.

Jafo akasema dhana ya ushindani na kumlinda mlaji zina uhusiano mkubwa na sababu kuwapo ushindani wenye afya katika soko.

Hivi sasa, Waziri Dk. Jafo yuko mkoani Mtwara na jana alikuwa wilayani Liwale. Alipotembelea mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa, ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa hatua za serikali za kuimarisha miundombinu ya sekta ya uvuvi nchini.

"Huu ni uwekezaji wa kwanza mkubwa katika bandari hii kubwa nzuri ya uvuvi, ambayo itabadilisha kabisa uchumi wa taifa letu hili katika sekta ya uvuvi.

"Ndani ya muda mfupi tukumbuke Mheshimiwa Rais ametoa (shilingi) bilioni 266 kwa ajili ya mradi huu na tunaona utekelezaji wake unakwenda vizuri." anasema Waziri Jafo, akipataja patafungua fursa za biashara nchini na kuongeza thamani ya mazao bahari.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack akaishukuru serikali kuiwezesha Halmashauri ya Kilwa kuwa kitovu cha bandari ya kwanza ya uvuvi ya kisasa na kueleza kuwa fursa hiyo itwapatia wavuvi soko la uhakika

Inaendelea Uk 14

BIASHARA

# Chereko Rufiji, mbaazi sasa zao la mnada, bei yaruka 300/- hadi 1,753.

**Na Yasmine Protace, Kibiti**

MBAAZI ni zao, linalolimwa maeneo mbalimbali ya mikoa hapa nchini, lakini wengi walilima zao hilo kama kitoweo.

Kutokana na kuona zao hilo kama ni kitoweo, hawakulitilia mkazo kwa kulilima kwa wingi, kutokana na sababu hawakujua kama linaweza baadae kuwa mkombozi wao.

Inaelezwa kuwa miaka ya nyuma, waliolima mbaazi waliuza kilo moja kwa shilingi 200 na uuzaji huo uliwafanya walimaji washindwe kulima zao hilo kwa wingi, wakibaki katika kuamua kulima kidogo ngazi ya kufanya kitoweo.

Hata hivyo, baada ya kuwapo mfumo wa kuuza mazao ya wakulima kwa kwa njia ya mtandao, ambao mfumo huo umeandaliwa na serikali umekuwa ukifanyika kwa njia ya minada ambao wakulima hukusanya mazao yao kupitia vyama vya msingi na kisha mazao hayo kuuzwa kwa njia ya mnada.

Hivi karibuni Meneja wa Chama cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU), Hamis Mantawela linakuja zao la, anasema baada ya kwisha kwa uuzwaji zao la ufuta katika mkoa wa Pwani, sasa ni msimu wa kuuza mbaazi na kisha korosho

Anasema, hata kama wakulima watakuwa wamelima mbaazi kidogo, anawasihi waikusanye katika maghala yao, ili ziuzwe katika mnada wanufaike na kujiongezea kipato.

" Tunajua mnaweza mkawa na mbaazi chache (kidogo) majumbani, nyie leteni katika mnada, huku bei itakuwa nzuri kuliko kuuza bidhaa hiyo kwa bei ndogo," anasema.

Anafafanua kuwa mkoa wa Pwani, zaidi ya tani 100 wamekusanya na matarajio ya mnada wa pili wamefanikiwa kuuza kilo moja ya mbaazi kwa shilingi 1,753.



Meneja wa CORRECU Mkoa wa Pwani, Hamis Mantawela, akipokea bei ya mnada wa mbaazi uliofanyika kwa njia ya mtandao kutoka kwa wanunuzi. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

Mantawela anasema ni jukumu la wakulima kuongeza uzalisha zao la mbaazi, ili waweze kunufaika nalo na katika miaka ya nyuma, mbaazi iliuzwa kilo moja shilingi 200 hadi 300, lakini mnada umefanyika na kuuzwa kwa bei hiyo mpya, shilingi 1753 kwa kilo moja.

Anasema kutokana na hali hiyo, wakulima wanatakiwa kuboresha kilimo chao, ili bei kuwezesha bei inaongezeka maradufu.

" Wakulima wanatakiwa kuboresha mashamba yao, ikiwamo kuboresha kilimo chao, ili waweze kunufaika kwa kuuza kwa bei kubwa," Mantawela anasema.

Anarejea katika mkoa wa Pwani, wakulima wake wamechelewa katika kilimo kukifanikisha kilimo cha mbaazi.

Mwenyekiti wa Chama Cha Msingi cha Ushirika (AMCOS) cha Ikwiriri AMCOS, Kassim Mpwele, anaeleza wanafurahi kilimo cha mbaazi kuingizwa katika biashara hiyo tajwa.

Kassim ambaye pia ni mwakikishi wa wakulima wa Kibiti CORRECU mkoani Pwani, akatumia nafasi hiyo kuwaahidi wakulima kuweka mbegu bora za mbaazi, ili mwakani wanufaike zaidi.

Anaeleza, zamani walikuwa wakilima mbaazi na kukifanya kitoweo pekee, saa anasifu mageuzi ya sasa kwa mkulima biashara ya mbaazi imekuwa nzuri zaidi.

**SAUTI YA WAKULIMA**

Amina Jumanne, Mkulima wa Mbaazi Kibiti, anaeleza kuishukuru serikali kuliona zao la mbaazi, nalo liuzwe kwa njia ya mnada, akitaka elimu itolewe zaidi kwa wakulima wa mbaazi wanufaike na mageuzi hayo.

Bakari Juma, mkulima wa ufuta na korosho anasema watu wamekuwa wakilima mbaazi majumbani ikiwa ni kitoweo, lakini mageuzi hayo mapya, sasa zao hilo likiingizwa katika mnada wa mauzo ya mazao, imani yake ni kwamba mwaka ujao wakulima wake wataongezeka, hata uzalishaji nao kutanuka .

" Zamani watu walielekeza nguvu katika ufuta na korosho, leo tena kuna zao la mbaazi, hivyo inatakiwa elimu itolewe, mwakani walime mbaazi kwa wingi," anasema.

Shaban Juma mkazi wa Kibiti pia mkulima wa ufuta, korosho na mbaazi, ana mtazamo wake kutaka elimu itolewe kwa wananchi waweze kunufaika na zao hilo.

Anasema kutokana na watu wengi kulima mbaazi kama kitoweo, sasa watalima kwa wingi kama zao la biashara.

## JAFO NA MCHAKAMCHAKA WA MAAGIZO 2 YA RAIS KAZINI VIWANDA, BIASHARA

Inatoka Uk 11

la Samaki la Pamoja, kuwawezesha wajasiriamali na wawekezaji kupata eneo maalumu la kupata malighafi.

**RAIS & BIASHARA KIMATAIFA**

Siku moja baada ya kutangaza mabadiliko ya nafasi katika wizara inayochukuliwa na Waziri Jafo, kwenye ufunguzi wa Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa, Rais Dk. Samia akatamka:

"Dk. Ashatu Kijaji ambaye nilimbadilisha kazi jana tu kabla ya leo, lakini natambua kazi kubwa aliyoifanya katika kutayarisha maonesho haya na kazi kubwa aliyoifanya katika kujenga Wizara ya Viwanda na Biashara..."

"Serikali itaendelea kufanya kila linalowezekana kusikiliza na kutatua changamoto za wafanyabiashara nchini. Kwa mfanyabiashara yeyote mwenye maoni ya kuboresha, kujenga na kuisadia nchi, milango ipo wazi.

"Waendelee kuwasiliana na mamlaka zetu mbalimbali ikiwamo wizara yenye dhamana ya biashara, bila kusahau taasisi yake ya TanTrade," akasema.

Maonyesho ya Sabasaba mwaka huu yamekutanisha kampuni 3,486, Rais akitaja ni ishara ya kukua na mvuto mkubwa wa biashara kimataifa, unaochangiwa na usimamizi thabiti wa serikali, ikiwamo sekta za Biashara, Viwanda na Uwekezaji.

"Ni ukweli usiopingika kuwa njia mojawapo ya kufikia azma hii ni uendelezaji na uimarishaji wa ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa, hivyo kufungua fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji. Matunda ya kuimarika kwa ushirikiano tumeshaanza kuyaona.

"Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa maana ya TIC kimesajili miradi 504 mwaka jana, yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 5.68.

"Hii ni kwa sababu watu wanakuja Tanzania, wanaona fursa, wanashiriki maonyesho, wanatembelea mabanda mengine na kuona fursa zilizopo Tanzania na kuvutika kuja kuwekeza," anasema.

Rais akataja tamwimu, kwamba mauzo ya nje ya bidhaa yalipanda kutoka shilingi trilioni 12.3 mwaka 2019 hadi kufikia shilingi trilioni 17.38 sawa na Dola za Marekani Bilioni 6.57 mwaka jana.

"Niwahakikishie kuwa tunaendelea kujenga, kuboresha na kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ya miundombinuili kuhakikisha tunaongeza tija kwa uzalishaji, kwa wingi na sifa 'quality' (ubora) na 'standards' (viwango).

"Vilevile, tuhakikishe kwamba tunakamilisha miradi ya miundombinu ili bidhaa zinazozalishwa ziweze kinasafirishwa kirahisi kufika kwenye masoko yanayokusudiwa.

"Vilevile, kazi hii tunayoifanya itaendelea kuwawezesha majirani zetu kunufaika kwa kutumia miundombinu hii katika kuchochea maendeleo ya ukuaji wa nchi zao. Ni kwa namna hii tutaendelea kuifanya Tanzania kuwa mahali sahihi pa Biashara na Uwekezaji," akatamka Rais.

**RAIS NA BIASHARA**

Akiwa mwaka mmoja tu madarakani, Rais Dk. Samia, moja ya ajenda zake 'alizozifungia kibwebwe' ni kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia sera, sheria na taratibu.

Hadi kufika mwaka 2022, Rais akatangaza salamu za tabasamu, kuongezeka pato la taifa kutoka shilingi trilioni 39.9 za mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 45.2 mwaka 2022.

Ilikuwa katika hotuba yake akifungua Mkutano wa 14 wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Ikulu, Dar es Salaam, akiitaja baraza hilo litaendelea kuwa moja ya vyombo rasmi vya kuishauri serikali kuhusu hatua za kuimarisha biashara, lengo ni kujenga uchumi shirikishi nchini.


Rais akaihimiza TNBC kufanya mashauriano yatakayoimarisha uwezo wa sekta binafsi nchini, kuzalisha bidhaa za huduma zitakazopunguza uagizaji na kuongeza mauzo katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Vilevile, akaitaja kuwa ni hatua wezeshi nchini kupunguza matumizi ya fedha za kigeni na kuongeza mapato, hata kuimarisha uchumi wa nchi.

Rais Samia akasema serikali inaendeela kuweka mkazo katika kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwamo miundombinu, nishati na Tekinaljia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), inayowezesha kukua biashara.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hii miti inavyokatwa ovyo, tutalia na kusaga meno huko tunakong'ang'ania







NA ADAM FUNGAMWANGO

KWA miaka ya hivi karibuni kumekuwa na tabia ya ukataji miti ovyo kwenye mikoa mingi ya Tanzania.

Ukataji miti huo uliokithiri umekuwa ukileta matatizo mbalimbali yakiwemo mabadiliko ya tabia nchi.

Ndiyo maana unaweza kukuta mabadiliko ya mvua, zamani ilikuwa ikinyesha miaka fulani, lakini sasa hainyeshi.

Mvua zinakuwa hazina tena kanuni, zinanyesha muda wowote, vyanzo vya maji vinakauka, wakati mwingine hata mito inabadililisha njia zake.

Unaweza kuona unabadilisha sura yake ya zamani, badala ya kupita kushoto inapita kulia. Kikubwa zaidi ni ukame. Ukataji ovyo wa miti unasababisha ukame, mara nyingi ukame husababisha wananchi washindwe kulima hali inayosababisha njaa.

Waswahili wana msemo wao 'maji ni uhai'. Wako sahihi kwa sababu unapokwenda popote pale, ili ujue kuwa sehemu hiyo ina uhai, yaani watu waishi eneo hilo, ni lazima ukutane na miti au mimea iliyo na rangi ya kijani kibichi na pili ni maji.

Kwa asilimia kubwa hapo maji na mvua ndiyo inasababisha mimea na miti iwe ya kijani. Maana yake ni kwamba mvua inanyesha eneo hilo. Na haiwezi kunyesha kama watu wanakata miti.

Mvua hupendelea kunyesha sehemu yenye miti mingi au misitu.

Hapo sasa unaweza kuona umuhimu wa kutunza miti, ambayo ndiyo inalinda vyanzo vya maji.

Zamani miaka ya nyuma, babu zetu walikuwa na uwezo mkubwa wa kulinda vyanzo vya maji kwa kutumia plani mbalimbali, ikiwamo kuweka mila na utamaduni.

Walikuwa wakiwaambia watoto wa vijana kuwa miti ile mikubwa ni sehemu ya matambiko ambayo hatakiwi mtu yoyote kupata miti kwani akifanya hivyo atapotea msituni.

Wakati mwingine wanaambiwa pori lina mizimu, au joka kubwa ambalo mtu akienda kwa sababu za uovu ikiwa pamoja na kukata miti, atakufa akiwa ndani ya msimu.

Ili kukata miti, wazee wenyewe waliitana na kufanya kitu kama tambiko ili kwenda kukata miti na walifanya hivi makusudi ili vizazi vijavyo viendelee na utamaduni huu.

Walijua kama wakiacha tu bila kuweka marufuku hiyo basi vijiji na maeneo yao yatabaki jangwa kutokana na mahitaji ya miti.

Akiwa Makete mkoani Njombe, Dk. Pindi Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii, aliwaonya wananchi wa Wilaya hiyo kuacha tabia ya kukata miti ovyo.

"Tusikate moto ovyo, tukikata tutakuwa jangwa, tukiwa jangwa tukakosa mvua, na tukikosa mvua tutakosa chakula," alisema Dk. Chana katika mkutano uliofanyika Kata ya Isapilano.

Alichosema Balozi Chana inabidi kizingatiwe siyo na watu wa Makete, au Njombe tu, bali Tanzania nzima.

Tumekuwa na kizazi ambacho kwa sasa hakina woga tena, huwezi kuwaambia kwenye msitu kuna joka, au mizimu wanakusikia.

Badala yake sasa kuna kizazi cha watu wanaohitaji elimu ili wafahamu madhara ya kukata miti au faida ya kutunza miti.

Kinachotakiwa sasa ni serikali kuanzia kuu mpaka ya vijiji kuelekeza elimu kwa wananchi ili kuwaeleza umuhimu huo.

Tukiwaambia mvua inayonyesha pamoja na kwamba inaletwa na Mungu, lakini inanyesha eneo ambalo misitu na miti yake imetunzwa vizuri.

Miti ambayo pia inaleta vyanzo vingi vya maji, na ikijumisha hayo yote nchi inakuwa na neema ya mazao ya chakula na biashara.

BIASHARA

## BILIONEA MOHAMED AL FAYED;

# Afariki umri miaka 94 kaelemewa kashfa ubakaji wafanyakazi wake

**Na Mwandishi Wetu**

NI simulizi mbaya, kinamama watano wanadai kubakwa na mmiliki wa zamani wa duka kubwa la kifahari la Harrods, Mohamed Al Fayed walipokuwa wakifanya kazi katika duka la London.

Ufuatiliaji wa Shirika la Habari Uingereza (BBC), umesikia kauli kutoka kwa wanawake zaidi ya 20 waliokuwa wafanyakazi, wanaosema bilionea huyo aliyefariki mwaka juzi akiwa na umri wa miaka 94, aliwanyanyasa kingono, ikiwamo ubakaji.

Ushahidi uliotolewa, unadai wamiliki wa sasa wa duka hilo wanaeleza kusikitishwa na matukio hayo na wanaomba radhi. Inatajwa, matukio hayo yametokea katika miji ya London, Paris, St Tropez na Abu Dhabi.

"Niliweka wazi kwamba sitaki. Sikutoa ruhusa," anasema mmoja wa wanawake hao, ambaye anasema Fayed alimbaka katika nyumba yake ya Park Lane.

Mwanamke mwingine anasema alikuwa msichana alipobakwa huko Mayfair, akitamka anachokita unyama akifafanua "wafanyakazi wote wa Harrods walikuwa kama vitu vyake vya kuchezea."

Fayed alikabiliwa na madai ya unyanyasaji wa kingono alipokuwa hai, lakini madai ya sasa ni makubwa zaidi katika rekodi zilizoko.



Mohamed Al Fayed. **PICHA: MTANDAO**

### SAFARI YAKE

Kazi ya ujasiriamali ya Fayed, alianza Alexandria, Misri, ambapo aliuza vinywaji vikali kwa wapita njia. Lakini ndoa yake na dada wa milionea, mchuuzi wa silaha wa Saudia ndiyo iliyomsaidia kuunda uhusiano mpya na kujenga himaya ya biashara.

Alihamia Uingereza 1974 na tayari alishakuwa mtu mashuhuri alipouchukua mradi wa Harrods mwaka 1985. Katika miaka ya 1990 hadi 2000, alionekana kila mara kama mgeni kwenye vipindi vya televisheni na burudani.

Fayed ndiye baba wa Dodi aliyefariki katika ajali ya gari akiwa pamoja na Princess Diana wa Wales, mwaka 1997.

Kinamama waliozungumza na BBC wanasema taswira yake ya kupendeza na urafiki ilikuwa mbali na uhalisia wake, huku mwanamama anayeitwa Sophia, aliyefanya kazi kama msaidizi wake binafsi kutoka 1988 hadi 1991, anasimulia alivyoangukia jaribio la kujaribiwa kubakwa zaidi ya mara moja.

Anatajwa Tajiri huyo Fayed, alikuwa na tabia ya kukagua kila mara ghorofa za chini, kuwatambua wafanyakazi wasichana wanaomvutia, baadaye anawapandisha cheo kufanya kazi katika ofisi zake za juu - wafanyakazi wa zamani, wanaume na wanawake, walituambia.

Unyanyasaji wake aliufanya katika ofisi za Harrods, katika nyumba yake ya London, au katika safari za nje - mara nyingi huko Paris katika hoteli ya Ritz, ambayo pia anaimiliki, katika jengo lake la Villa Windsor.

### SIMULIZI 'ALINIBAKA'

Rachel, sio jina lake halisi, alifanya kazi kama msaidizi wake binafsi katika duka la Harrods katika miaka ya 1990.

Usiku mmoja baada ya kazi, anasema alimwita kwenye nyumba yake ya kifahari, huko Park Lane. Jengo hilo lilikuwa likilindwa na wafanyakazi wa usalama.

Rachel anasema, Fayed alimtaka aketi kwenye kitanda chake kisha akaweka mkono wake mguuni, akiweka wazi anachotaka.

Hija za kinamama wengine 13, wanalalamika ambao wanasema Fayed aliwanyanyasa kingono katika nyumba ya 60 Park Lane. Wanne kati yao, akiwamo Rachel, wanasema walibakwa.

Sophia anasema alinyanyaswa kingono akitamka: "Sikuweza kuondoka. Sikuwa na familia ya kurudi, nilitakiwa kulipa kodi."

Gemma, aliyefanya kazi kama mmoja wa wasaidizi wa binafsi wa Fayed kati ya 2007-09, anasema tabia yake ilitisha zaidi wakati wa safari za kikazi nje ya nchi.

Anasema alibakwa katika nyumba Villa Windsor huko jijini Paris - nyumba ya zamani ya Mfalme Edward VIII na mkewe Wallis Simpson.

Anasema baada ya Fayed kumbaka alilia. Fayed alinyanyuka na kumwambia kwa ukali akaoge na sabuni maarufu (jina tunalo).

"Ni wazi alitaka nifute ushahidi wowote wa yeye kuwa karibu nami," anaeleza, na kuna wanawake wengine wanane, pia wametuambia walinyanyaswa kingono na Fayed huko Paris. Wanawake watano walitaja unyanyasaji huo kama jaribio la ubakaji.

SIRI HADHARANI

"Unyanyasaji wa wanawake niliufahamu nilipokuwa dukani," anasema Tony Leeming, Meneja wa Harrods kutoka 1994 hadi 2004, akinena "haikuwa siri." Hata hivyo anasema, hakujua kuhusu madai mazito ya ubakaji.

Kauli ya Leeming inaungwa mkono na wanachama wa zamani wa Timu ya Usalama ya Fayed wakinena: "Tulifahamu alikuwa akipenda sana wasichana wadogo."

Eamon Coyle, alijiunga na Harrods mwaka 1979 kama Mpelelezi wa Duka, kisha akawa Naibu Mkurugenzi wa Usalama kuanzia mwaka 1989 hadi 1995.

Steve ambaye siyo jina lake halisi anasema alifanya kazi kwa bilionea huyo kati ya mwaka1994 na 1995 na aliwadokeza wafanyakazi wa usalama mambo yao ya siri, kwa wafanyakazi kadhaa wa kike huko Harrods na Park Lane."

Wanawake wote waliozungumza walieleza kuwa hofu ndiyo ilifanya iwe vigumu kwao kuzungumza, huku Sarah, ambaye si jina lake halisi, anasema:

"Hakika kulikuwa na utamaduni wa hofu katika duka zima - kutoka watu wa hali ya chini, hadi wakuu."

### SIMU KUFUATILIWA

Wengine wakasema waliamini simu katika duka la Harrods zilifuatiliwa na wanawake walikuwa wakiogopa kuzungumza wao kwa wao kuhusu unyanyasaji wa Fayed, wakihofia kuwa walikuwa wakirekodiwa na kamera zilizofichwa.

Aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Usalama, Eamon Coyle, akathibitisha, miongoni mwa majukumu yake ilikuwa ni kusikiliza mazungumzo ya simu yaliyorekodiwa. Kamera ambazo zinaweza kurekodi pia ziliwekwa kwenye duka lote, alisema, pamoja na vyumba vya watendaji.

Harrods inasema katika taarifa yake kwa BBC kuwa haya yalikuwa ni matendo ya mtu "mwenye nia ya kutumia vibaya mamlaka yake" na inalaani vikali.

"The Harrods ya leo ni shirika tofauti sana na lile lililomilikiwa na kudhibitiwa na Al Fayed kati ya 1985 na 2010, ni shirika ambalo linaweka ustawi wa wafanyakazi wake katika kila kitu inachofanya."

### SIRI KUFICHULIWA

Kulikuwapo majaribio ya kufichua tuhuma dhidi ya Fayed kabla ya kifo chake, moja kupitia jarida la Vanity Fair mwaka 1995, katika makala iliyoeleza ubaguzi wa rangi, ufuatiliaji wa wafanyakazi na tabia mbaya za ngono. Lakini Fayed alifungua kesi ya kashfa.

Mohamed Al Fayed, baadaye alikubali kufuta kesi hiyo ikiwa ushahidi uliokusanywa na gazeti hilo kuhusu utovu wake wa kingono utafutwa.

Mwaka 1997, The Big Story ya ITV iliripoti madai mengine ikiwamo unyanyasaji wa kijinsia na kupapasa.

Mmoja wa wanawake katika uchunguzi wa BBC, Ellie, sio jina lake halisi, alikuwa na umri wa miaka 15 mwaka 2008 aliporipoti unyanyasaji kwa polisi - madai ambayo yalichukua vichwa vya habari - lakini haikusababisha mashtaka yoyote.

Mwaka 2017, televisheni Channel 4 iliripoti madai ya kupapasa, kushambulia na kunyanyasa, mwanamke huyo alikuja hadharani na iliwapa wanawake wengine ujasiri wa kujitokeza - na uchunguzi wa 2018 kwenye Channel 4 News ulifanyika.

Tangu Mohamed Al Fayed kufariki mwaka jana, wanawake wengi zaidi wameweza kuzungumza hadharani kuhusu ubakaji na jaribio la ubakaji.

### MAPATANO

Inatajwa, sehemu ya suluhu ya mwaka 2009 ni simulizi ya mwanamama Germma kutia saini makubaliano ya kutofichua tuhuma hizo, mkataba unaomzuia kisheria na unaohakikisha habari inabaki kuwa siri.

Anasema baada ya kubakwa, aliwasiliana na wakili ambaye alimwambia kuwa anaacha kazi kwa sababu za unyanyasaji wa kijinsia.

Kampuni Harrods ilikubali, anaweza kuondoka na kumlipa madai yake, lakini asivujishe ushahidi na badala yake asaini makubaliano hayo. Gemma anasema mfanyakazi wa ofisi ya rasilimali watu (HR) kutoka Harrods alikuwepo wakati makubaliano yakifanyika.

BBC imeelezwa na wanawake waliotishwa na mkurugenzi wa usalama wa wakati huo wa Harrods, John Macnamara, ili kuwazuia wasizungumze.

Wanawake kumi na wanne tuliozungumza nao wamefungua mashitaka dhidi ya Harrods wakitaka fidia. Wamiliki wa sasa wa duka, walianza kusuluhisha kesi hizi mwezi Julai 2023.

Ilimchukua Sophia na Harrods miaka mitano kufikia makubaliano. Wanawake wengi zaidi sasa wanatarajia kuchua hatua za kisheria dhidi ya Harrods.



HABARI DODOMA

# Serikali, TLS wakutana wajadili Katiba Mpya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi na Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili wa Tanzania (TLS) wamekutana kujadili mambo yanayohusu sekta ya sheria ikiwamo suala la Katiba.

Mambo yaliyojadiliwa ni kuendelea kuimarisha utawala wa sheria na TLS kushirikiana kwa karibu kwenye Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Tume ya Kurekebisha Sheria na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Katika majadiliano hayo yalitanguliwa na kikao cha menejimenti ya wizara ikiongozwa na Katibu Mkuu Eliakim Maswi kwa lengo la kujadili masuala ya kitaalamu na baada ya hapo kilifuata kikao cha awamu ya pili kilichomjumuisha Waziri Kabudi.

Akizungumza baada ya kikao, Waziri Kabudi alisema wamejadili mambo mengi kwa muda mrefu na yote yamekuwa na manufaa katika ustawishaji wa demokrasia kupitia sekta ya sheria, huku akisema wameanza vizuri na uongozi mpya wa TLS.

Alisema wamejadili mambo mengi yanayohusu Katiba na kwamba TLS wamesema baadhi ya vifungu vya Katiba wamevielewa vizuri na wataenda kuelewesha zaidi.

"TLS imeelewa kazi kubwa inayofanywa na Wizara kikubwa ambacho wamesisitiza ni ushirikishwaji zaidi ili baadhi ya maamuzi yanayofanyika washirikishwe na kuyafahamu na kuyaeleza," alisema.

**"TLS imeelewa kazi kubwa inayofanywa na Wizara kikubwa ambacho wamesisitiza ni ushirikishwaji zaidi ili baadhi ya maamuzi yanayofanyika washirikishwe ..**

Kuhusu msaada wa kisheria, Waziri kabudi alikubali ombi la wanachama wengi zaidi ya TLS kushiriki kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC) na kuagiza iundwe kamati ya pamoja itakayojumuisha wanachama wa TLS na kuangalia namna bora zaidi ya kuboresha utekelezaji wa kampeni hiyo.

Alifafanua kuwa wamekubaliana na TLS msaada wa kisheria uwe wa aina mbili yaani kutatua matatizo ya kisheria na kutoa elimu ya kujua sheria kwa wananchi.

Alisema: "Kampeni hii ya Mama Samia sasa itakuwa na mambo hayo mawili kuwasaidia watu katika changamoto zao na pili kuanza kutoa elimu ya sheria ili wananchi waelewe haki zao, wajibu na sheria inafanya nini."

Pamoja na hilo, jambo lingine lilijadiliwa ni uanzishwaji wa Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi ambacho kitakuwa chombo cha kimataifa ambacho kitaweza kuhudumia watu wa nchini na kutoka mataifa mbalimbali, ambapo Waziri Kabudi alielekeza iundwe kamati na uandaliwe mpango mzuri juu ya uanzishwaji wa kituo hiko.

Rais wa TLS Mwabukusi alisema amefarijika kwa kiasi kikubwa na namna mjadala ulivyoendesha na kwamba huo ni mwanzo mzuri na masuala yanayowahusu wananchi kisheria yatapatiwa ufumbuzi na yanayohitaji utafiti yaanze kufanyiwa kazi.



Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Gaspar Mgimiloko, akitoa maelezo kwa wakulima na maofisa ugani wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida yanayotolewa na taasisi hiyo lengo kuongeza uzalishaji wa zao hilo.**PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Ujenzi Bandari Mbambabay kufungua mkoa kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbambabay utakaogharimu Sh. bilioni 81, utaufungua mkoa kiuchumi kwa kuuza bidhaa mbalimbali nchi za Malawi na Msumbiji.

Kanali Ahmed alisema hayo jana alipokuwa akikagua utayari wa wilaya za mkoa huo kuhusu ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan na kilele cha Tamasha la Kitaifa la Tatu la Utamaduni litakalofanyika Uwanja wa Majimaji Manispaa ya Songea.

Alisema serikali imeelekeza fedha hizo zitekeleze mradi huo ikiwa ni miongoni mwa miradi mikubwa itakayoipaisha Ruvuma kiuchumi.

Alisema ujenzi wa bandari hiyo ukikamilika utasaidia kutoa ajira, kuinua uchumi, kupeleka na kupokea bidhaa mbalimbali ikiwamo mazao, samaki na bidhaa za viwandani katika nchi jirani za Malawi na Msumbiji.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kuleta fedha nyingi kutekeleza miradi mbalimbali inayogusa wananchi wetu kwenye sekta ya afya, elimu, miundombinu kama unavyoona hapa kutajengwa bandari hii ambayo Sh.bilioni 81 zimetolewa kutekeleza mradi huu," alisema.

Aidha, alikagua Barabara ya Mbinga hadi Mbambay ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami na kwamba barabara hiyo itafungua uchumi wa mkoa huo kwa kuwa ni kiunganishi kati ya Tanzania, Malawi na Msumbiji.

Alisema mkoa huo umejiandaa kumpokea Rais Samia katika ziara yake itakayoambatana na matukio mbalimbali ikiwamo Tamasha hilo.

Alibainisha kuwa ziara ya Rais Samia inalenga kukagua miradi ambayo mkoa huo umepokea fedha nyingi kuitekeleza katika sekta mbalimbali.

# TEHAMA yapunguza mlundikano mashauri mahakamani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MATUMIZI ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye mhimili wa mahakama nchini yametajwa kusaidia kupunguza mlundikano wa mashauri kutoka asilimia 10 hadi tatu mwaka 2023.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel alibainisha hayo jana jijini hapa, wakati akizungumza kwenye kikao kati ya Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) na mahakama.

Prof. Ole Gabriel alisema takwimu hizo hutolewa na taasisi ya REPOA ambao wamekuwa wakifanya utafiti.

Aidha alisema tathmini hiyo hutolewa kila baada ya miaka minne na taasisi hiyo, hivyo suala la matumizi ya TEHAMA katika muhimili huo linazidi kupunguza msongamano mahakamani.

"Tuna shukuru matumizi ya TEHAMA katika mahakama kunasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mlundikano wa mashauri tunaendelea kutumia TEHAMA ili kurahisisha uendeshaji wa kesi,"alisema Profesa Ole Gabriel.

Alisema wanasubiri tathmini nyingine ambayo itatolewa baada ya miaka minne na kuongeza kuwa wanaishkuru serikali kwa kuwekeza katika mahakama.

Mbali na hilo alisema wamepokea ombi la TLS la kuwataka mahakama kutoa elimu kwa mawakili kuanzia ngazi za juu hadi chini ili kusaidia wajue mifumo inayotumika.

Kadhalika, alisema wamelipokea na watalifanyia kazi ili kuhakikisha uhusiano wao unakwenda vizuri katika masuala ya kisheria.

Hata hivyo, alisema wamealikwa kwenda Marekani ili kuelezea namna wanavyotumia mikopo nafuu katika uwekezaji wa miundombinu ya mahakama uliosababisha kupunguza mlundikano wa kesi.

Alisema mwaliko huo ni hatua kubwa kwao na kuongeza kuwa utazidi kupanua wigo wa ufanyaji kazi ya mahakama.

Vile vile, alisema watasaini makubaliano kwa ajili ya kushirikiana na Baraza la TLS ili kuhakikisha kila mmoja anapata haki yake.

Rais wa TLS, Boniface Mwabukusi alisema wameiomba mahakama kutoa elimu zaidi kwa mawakili ili waweze kukaa pamoja katika masuala ya kisheria na utendaji kazi.

Alisema wamewasilisha ombi hilo ili kuona kama litafanikiwa ili iwe rahisi kwao kufanya kazi zao kwa urahisi kutokana na kuwa kila siku wanakutana na kesi.

Mwabukusi alisema mahakama ni sehemu ya kupata haki hivyo anaye ilalamikia mahakama anahitaji kuchunguzwa. Hata hivyo alisema anaamini ushirikiano huo utakwenda kuleta matokeo chanya kwa jamii kwenye masuala ya kisheria nchini.





# Wazee watakiwa kuwaonya vijana kuhusu maadili

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

WAZEE nchini wametakiwa kuwaonya vijana wanaokwenda kinyume na tamaduni za kitanzania kwa kufanya vitendo vinavyosababisha mmomonyoko wa maadili.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Mlezi wa Mkoa wa Njombe, Halima Mohamed Mamuya alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na wanachama wa chama hicho kutoka Tarafa ya Imalinyi wilayani Wang'ing'ombe.

Mamuya aliwataka wazee kutojitoa katika suala la malezi kwa sababu l ipo wimbi la vijana linaloendelea kuteketea kutokana na kukosa maadili.

"Wazee msijitoe katika malezi, utaona hata katika viongozi wa dini wengine wameacha yale maandiko mengine yaliyoandikwa katika vitabu wanasema sasa yale ya siasa," alisema Mamuya.

baadhi ya wanachama walioshiriki mkutano huo walisema suala la maadili linatakiwa lianze kusisitizwa kuanzia ngazi ya chini ikiwemo shule za msingi na sekondari.

Mmoja wa wanachama hao, Julius Mgao alisema mambo mapya mengi yanakuja, hivyo kijana anapaswa kuelimishwa kuhusu suala zima la utandawazi.

**"Kuna utandawazi vijana wadogo kabisa wanasimu janja, hivyo ni wajibu wetu sasa kuanza kuwaelimisha mapema kabla hajakutana na hivi vitu vya kisasa," alisema Mgao.**

"Kuna utandawazi vijana wadogo kabisa wanasimu janja, hivyo ni wajibu wetu sasa kuanza kuwaelimisha mapema kabla hajakutana na hivi vitu vya kisasa," alisema Mgao.

Mbunge wa Wanging'ombe ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) (sekta ya afya), Festo Dugange alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewapatia fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya Imalinyi ambazo ni Sh. milioni 500.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Zakaria Mwansasu alisema tayari wamepokea zaidi ya Sh. bilioni sita kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Alisema miradi hiyo iko katika sekta ya elimu, afya, miundombinu ya barabara, kilimo na sekta zingine ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi.

Katibu wa CCM Mkoa wa Njombe, Julius Peter aliwataka wanachama hao kuyazingatia maelekezo ya chama kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuibuka na ushindi.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam, akitafuta vipande vya nondo kwenye zege lililobanduliwa katika mtaro wa barabara ya Morogoro eneo la Kimara Baruti jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakulima wakoshwa mfumo uendeshaji minada

**Na Gideon Mwakanosya,**
TUNDURU

WAKULIMA wa mbaazi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamesema mfumo wa wazi wa uendeshaji wa minada ya zao hilo unasaidia kuondoa migogoro baina yao na wanunuzi.

Walisema hayo juzi wakati wakizungumza na Nipashe kwenye mnada wa pili wa mbaazi, ambapo baadhi ya wakulima akiwemo, Ania Mohamed alisema wakulima wanafurahishwa na uendeshaji wa minada ya zao hilo ambayo hufanyika sehemu ya wazi.

Naye Salima Adamu aliiomba serikali kusimamia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kuwa mfumo huo unawanufaisha wakulima wa kipato cha chini kwa kupata bei nzuri ya mazao yao.

Alisema awali wafanyabiashara waliozoea kuwanyonya wakulima kwa kununua mazao kwa bei ya chini.

Kaimu Meneja Mkuu wa Chama Kikuu Cha Ushirika wa Wakulima Tunduru (TAMCU), Zainabu Sendema alisema chama kikuu kitaendelea kufanya minada yote sehemu ya wazi ili kutoa nafasi kwa wakulima kushiriki kwa wingi na kutoa maamuzi ya bei ya kuuzia mazao yao.

Hata hivyo Sendema alisema katika mnada wa pili wa soko la mbaazi kilo milioni 3.5 ziliuzwa kwa bei ya wastani wa Sh.1718.

Sendema aliwashauri wakulima wa Wilaya ya Tunduru kulima mazao mbalimbali badala ya kutegemea zao moja ambalo linachelewesha maendeleo.

# Bil.81/- zatengwa ujenzi wa bandari Mbambabei

**Na Mwandishi Wetu,**
RUVUMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 81 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbambabay katika Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, aliyetembelea eneo la ujenzi wa bandari hiyo akiambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kama sehemu ya maandalizi ya mapokezi ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Rais Samia anatarajiwa kuwasili mkoani Ruvuma Septemba 23 mwaka huu kwa ziara ya kikazi ambapo pia ataanza kwa kuzindua Tamasha la Kitaifa la Utamaduni litakalofanyika wilayani Songea.

Kanali Abbas alisema ujenzi wa bandari hiyo ukikamilika utasaidia kutoa ajira, kuinua uchumi, kupeleka na kupokea bidhaa mbalimbali ikiwemo mazao, samaki na bidhaa za viwandani katika nchi za Malawi na Msumbiji.

Alisema baada ya kuzindua tamasha la utamaduni Rais Samia atatembelea wilaya mbalimbali za Mkoa wa Ruvuma kuangalia shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo miradi ya barabara ambazo zimejengwa kwa viwango vya kimataifa.

Tamasha hilo la utamaduni linatarajiwa kuhudhuriwa na watu zaidi ya 5,000, hivyo kuwa fursa kubwa ya kiuchumi kwa wananchi wa mkoa huo kutokana na shughuli za kiuchumi zitakazokuwa zikifanyika kwa siku hizo nne.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro alisema tamasha hilo litaanza Septemba 20-23, mwaka huu na siku ya kilele kitafanyika Uwanja wa Majimaji na Rais Samia Suluhu Hassan atakuwa mgeni rasmi.

Alisema tamasha hilo litajumuisha maonesho ya mavazi ya asili ikiwamo kanga, vyakula, ngoma kama vile mganda na lizombe.

Alibainisha kuwa Rais Samia atakutana na wazee wa kimila na kuzungumza nao kwa kuwa mkoa huo unahistoria mbalimbali kama vile vita ya majimaji kwa kutembelea kaburi la halaiki la mashujaa wa majimaji.

Alisema Rais Samia atahitimisha ziara Septemba 28, mwaka huu kwa kufanya mkutano wa ndani wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na mkutano wa hadhara kwa wananchi kwenye Uwanja wa Majimaji.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Jenista Mhagama, Meliud Mwampembe alisema shule hiyo imetoa kipaumbele kwa masuala ya michezo na utamaduni kwa wanafunzi.

Alisema: "Hili jambo la utamaduni na michezo ni la msingi kwa sababu linatunza asili yetu sisi kama Watanzania, ninahamasisha sana wananchi kushiriki katika tamasha hili linaloonesha tamaduni zetu lakini na fursa mbalimbali zilizopo Ruvuma".



# Ujenzi majengo ya mahakama wafikia asilimia 45

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema kasi ya ujenzi wa majengo ya mahakama za mkoa na wilaya kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) umefikia asilimia 45.

Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza ufanisi wa usikilizaji wa mashauri yanayowakabili wananchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa maagizo yaliyotakiwa kufanywa na Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023-2024 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu miongoni mwa vipaumbele vya serikali ni kuona mfumo wa usikilizaji wa kesi unapatiwa ufumbuzi ikiwemo kuajiri mahakimu na majaji wa kutosha.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu zaidi ya majaji 10 wameteuliwa kushika wadhifa huo, hatua ambayo imesaidia kuwepo kwa usikilizaji wa mashauri yanayowakabili wananchi kwa kasi kubwa.

Aidha alisema mahakama maalumu ya matukio ya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto imeanzishwa ambayo imesaidia kuwepo kwa kasi ya usikilizaji wa kesi zinazohusu kundi hilo.

**Kadhalika, alisema Serikali ya Zanzibar imeanza uchunguzi wa miradi ya maendeleo 70 na kubaini kuwepo kwa kasoro za kiutendaji zinazohusu ubadhirifu wa mali ya umma.**

Alisema kwa mara ya kwanza katika Kisiwa cha Pemba yupo Jaji wa Mahakama Kuu anayesiliza kesi zinazohusu matukio ya mauaji pamoja na rufaa zinazowahusu wananchi, hatua ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuondosha malalamiko yaliyokuwepo awali.

Kadhalika, alisema Serikali ya Zanzibar imeanza uchunguzi wa miradi ya maendeleo 70 na kubaini kuwepo kwa kasoro za kiutendaji zinazohusu ubadhirifu wa mali ya umma.

Akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir aliyetaka kujua kazi za uchunguzi zinazofanywa na Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) katika miradi ya maendelezo zimefikia wapi.

Waziri Suleiman alisema serikali imejipanga kuhakikisha miradi yote ya ujenzi wa maendeleo inafanyiwa uchunguzi kuona fedha halisi na thamani yake inavyozingatia ubora wake.

Alisema miradi 72 ya maendeleo yenye thamani ya Sh.bilioni 784 imefanyiwa uchunguzi na kutolewa ushauri baada ya kuonekana kasoro mbali mbali za ujenzi wake.

Alisema miradi mitano imebainika kuwa na kasoro ambazo zimebainika kuwepo kwa maosa ya kijinai, kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wahusika wake.



Mwakilishi wa jimbo la Kikwajuni, Nassor Jazira akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani nje ya mji wa Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil.1.4/- zatengwa kukabili athari mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetenga Sh.bilioni 1.4 kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023-2024.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman wakati akijibu swali la mwakilishi wa Malindi, Ahamed Ahmada aliyetaka kujua serikali imetenga kiasi gani katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akijibu swali hilo, Harusi alisema serikali imejidhatiti kupambana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi pamoja na athari zake ambazo ni kubwa kimazingira.

Aliitaja mikakati hiyo ikiwemo serikali kuzindua Kampeni ya Zanzibar ya Kijani ambayo imelenga kuotesha miti ya aina mbalimbali, lengo likiwa ni kukabiliana na athari za kimazingira katika maeneo ya ukanda wa fukwe za bahari.

Alisema kampeni hiyo tayari imeanza kufanya kazi ambayo ni kuotesha miti aina ya mikoko na mikandaa ambayo ni maarufu kwa kuzuia kasi ya maji ya bahari kuathiri maeneo ya fukwe za Unguja na Pemba.

Aidha, alisema elimu imeanza kutolewa na kufikisha ujumbe wa kulinda mazingira kupitia shule za msingi na sekondari.

Kuhusu Kisiwa cha Pemba, alisema tayari kampeni ya kukifanya kisiwa hicho kupambana na athari za mazingira imeanza ambayo ni kuotesha miti maarufu iliopo katika tishio la kupotea.

Aliitaja miti hiyo ni minazi ambayo ipo katika tishio la kutoweka kutokana na kasi ya wananchi kujenga nyumba na matokeo yake hulazimika kuikata.

Aidha alisema baadhi ya maeneo ikiwepo ya pembezoni mwa fukwe serikali inakusudia kujenga kuta ili kuzuia kasi ya maji ya bahari.

Alisema serikali imejenga ukuta katika eneo la Forodhani liliopo katika Mji mkongwe ambalo awali lilikuwa limeathirika na kasi ya maji ya bahari.

## Mipango yawekwa kumaliza ugonjwa wa vikope

**Na Halfani Chusi**

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, John Jingu amesema serikali imeweka mipango madhubuti kuhakikisha inamaliza ugonjwa wa vikope, ambao ni kisababishi kikubwa cha upofu.

Alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipokutana na mke wa Mwana wa Mfalme wa Uingereza, Sophie Helen aliyekuja nchini kuangalia mafanikio ya Tanzania katika kupambana na ugonjwa huo.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya imefanikiwa kudhibiti ungonjwa huo na kwamba katika halmashauri zote nchini tisa pekee bado kuna shida kidogo.

"Tumefanikiwa kwa asilimia 10 katika hizo halmashauri ambazo kuna shida kidogo tumeweka mikakati mbalimbali ya kutokomeza ikiwamo kutoa elimu, kuwajengea ufahamu wananchi ili wanapoona dalili waweze kuzitambua na kufika hospitali mapema" alisema.

Alisema katika hospitali zote nchini huduma na vifaa tiba vya ungonjwa huo vinapatikana na hivyo wenye dalili wafike hospital kwa matibabu.

Akizungumzia ujio wa ugeni huo, alisema ni ishara ya kuonyesha kuwapo kwa ushirikiano Katika ya Tanzania na Uingereza pia kumesaidia kuipatia nchi rasilimali fedha kwa ajili ya mambo mbalimbali katika sekta ya afya.

Balozi wa Uingereza nchini, Marianne Young, alisema wataendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika sekta ya afya.

Akizungumza na waandishi wa habari, Sophie alisema amekuja nchini kujadiliana na serikali kuhusu kuboresha zaidi huduma kwa magonjwa yasiopewa kipaumbele ikiwamo vikope.

Alisema hii siyo mara ya kwanza kuja Tanzania kusherehekea ushirikiano wa Uingereza na Tanzania kuhusu afya, kilimo na uwezeshaji wa wanawake.

Alisema watasafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar na Arusha kujadiliana na serikali na wadau mbalimbali wa afya ikiwa ni pamoja na mashirika ya kimataifa kuhusu watu wenye upofu.

Alisema katika ziara hiyo wametembelea Kituo cha Afya cha Magomeni jijini Dar es Salaam ambacho kinatoa huduma ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika Sightsavers, Godwin Kabalika alisema la hafla hiyo ilikuwa ni kuzuia upofu unaoweza kuzuilika.

Alisema ujio wa ugeni huo umekuwa kitu kizuri kwa sababu malkia huyo amekuwa na mchangao mkubwa katika magonjwa ya macho.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 344 LA 2024**
**SALIM MBAROUK............MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **MARIA B. MOMBA**
- **ARON EVAREST......MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

- **MARIA B. MOMBA**
- **ARON EVAREST............POPOTE ULIPO/MLIPO**

**SALIM MBAROUK** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 24/09/2024 saa 03:00 asubuhi/mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 18 Mwezi 09/2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TUMAINI GRAYSON CHIWINGA** ANATAGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI MC 533 BVT,CHASISI NAMBA MD2A21BZ1GWJ59045 ILIYOPOTEA KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI

**TAARIFA PHQ/IRI/IRI/14310/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALUA KAUMBYA SADICK** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0299/0592** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MKUGWA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/41410/2024.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 31/2024**
**MALISELA DESDERIUS SANGA...MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**ZOOH MOHAMED KISALELE.........MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi unatarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja sikiu ya tarehe 04/10/2024 saa 3:00 asubuhi. Shauri linakuja kwa ajili ya kusikilizwa.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikilizwa shauri bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo nami na mhuri wa Baraza hii leo tarehe 09/09/2024.

MWENYEKITI

**THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**BY THIS DEED POLL** I, the undersigned **JOSEPHINE NELSON NGOLOKA** of **P.O. Box SONGEA, 0784 739 648** Tanzania **DO HEREBY** absolutely renounce and abandon the use of my former names of **JOSEPHINE NELSON SANGA** and lieu thereof assume the name of **JOSEPHINE NELSON NGOLOKA.**

**AND IN PURSUANCE** of such change of name as aforesaid, I hereby declare that I shall, at all time hereafter in all records, deed and instrument, in writings and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions whatsoever use and sign the said name of **JOSEPHINE NELSON NGOLOKA** as my name in lieu of the former name of **JOSEPHINE NELSON SANGA** so renounced.

**AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUEST** all person to designate and address me by such assumed name of **JOSEPHINE NELSON NGOLOKA** only.

I, the said **JOSEPHINE NELSON NGOLOKA** make this declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the provisions of Oaths, (Judicial Proceedings) and Statutory Declaration Act, 1966.

**IN WITNESS WHEREOF**, I have executed this deed on the 10th day of **SEPTEMBER, 2024.**

SIGNED and DELIVERED by the said JOSEPHINE NELSON NGOLOKA who is identified to me by .................... and latter known to me personally in my presence this 10th day of SEPTEMBER, 2024. — DEPONENT



BEFORE ME:
NAME: EDMUND MNYAWAMI
SIGNATURE: ...............
ADDRESS: 937 SONGEA
COMMISSIONER FOR OATHS

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MBARALI**
**LILILOPO RUJEWA**
**MAOMBI NA 56 MWAKA 2023**
**MLETA MAOMBI: VAILETH MBILINYI**
**DHIDI YA**
**MJIBU MAOMBI:CHESANI NZIKU**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA:CHESANI NZIKU**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 16 Mwezi wa 10 Mwaka2024 saa08:00asubuhi mbele ya MH A.Mapunda Mwenyekiti wa baraza.Hivyo unaamriwa mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa

Fahamu kwamba unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi/majibu ya rufaa ndani ya siku ishirini na moja au/ na kiapo kinzani ya siku saba(7)

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu lakiri /mhuri wa baraza hili leo tarehe 19 Mwezi 08 Mwaka2024

................................
**MWENYEKITI WA BARAZA**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**REGINA JOHN ZUMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA TAE 319113 KILICHOTOLEWA NA TASISI YA UHAMIAJI MKOA WA MBEYA KWA YOYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

**TAARIFA YA POLISI: PHQ/MBE/MBE/28443/2024.**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Waathirika wa mauaji Guinea wafarijika kukamatwa Pivi

**CONAKRY, Guinea**

WAATHIRIKA wa mauaji nchini Guinea wameonesha kufarijika baada ya kukamatwa kwa Kanali Claude Pivi, aliyekuwa akitafutwa kutokana na kuhusika na uhalifu wa kibinadamu uliosababisha mauaji katika taifa hilo.

Ilielezwa kuwa Kanali Pivi alikuwa akitafutwa baada ya kuhukumiwa mwezi Agosti kwa uhalifu dhidi ya ubinadamu katika mauaji ya Septemba 28, 2009 katika uwanja wa Conakry na kwamba kwa sasa anashikiliwa na idara za usalama nchini Liberia.

Ilielezwa kuwa vyama vya waathiriwa na watetezi wa haki za binadamu wanasubiri ofisa huyo arejee Guinea ili aweze kutumikia kifungo chake.

Asmaou Diallo, ambaye ni rais wa shirika la waathiriwa wa Septemba 28, 2009, alisema kukamatwa kanali huyo ni faraja kubwa kwao.

"Pivi alipoondoka Conakry, ilizua wasiwasi mkubwa miongoni mwa waathiriwa. Atarudishwa nchini lini? Hakika tumeridhishwa sana na habari hii," alisema.

Mashirika ya waathiriwa wa mauaji hayo na wale wanaotetea haki za binadamu walikaribisha hatua ya kukamatwa kwa mtu huyo waliodai kuwa ni hatari kwao

"Ni lazima aadhibiwe kwa mujibu wa sheria. Alipendelea kukimbia kuliko kusikilizwa ipasavyo, na tumefarijika sana na hatua hiyo ya kukamatwa," alisema Asmaou Diallo kutoka shirika la Avipa.

Msemaji wa shirika la kutetea haki za binadamu nchini Guinea, Alseny Sall, alisema kukamatwa kwa Pivi ni habari njema kwakuwa inawahakikishia waathiriwa.

Alisema hata kama anataka afungwe nchini Guinea, alisisitiza kwamba taratibu lazima ziheshimiwe: "Yeye ni mmoja wa washtakiwa wakuu wa matukio ya 2008 na kwamba mwisho wa kesi, alitiwa hatiani.

"Ni dhahiri, tunaomba mamlaka ichukue hatua zote kuhakikisha haki yake inaheshimiwa, lakini pia anajibu kwa kile anachotuhumiwa.

"Kuhusiana na hili, itabidi tuwaachie mawakili wake watekeleze wajibu wao wakati wa utaratibu, lakini ni muhimu kwamba arudishwe Guinea na atumike kifungo chake pamoja na wengine walio katika gereza kuu la Conakry," alisema.

Pia ilielezwa kuwa kanali huyo alitoroka katika gereza alikowekwa awali na kwamba baada ya kukamatwa atarudishwa humo.

Pia ilielezwa kuwa kati ya Guinea na Liberia, kuna ushirikiano wa mahakama kupitia polisi ya kimataifa ya Interpol.

Miaka miwili ya kesi, hatia ya uhalifu dhidi ya ubinadamu, kifungo cha maisha, mamlaka ya Guinea ilikuwa imeahidi zawadi ya euro 50,000 kwa yeyote ambaye atasaidia katika kukamatwa kwake.

*RFI*



Wananchi Darfur ambao ni wakimbizi wanaotajwa na Umoja wa Mataifa (UN) kuwa wako hatarini, huku Ofisa mwandamizi wa umoja huo akionya kwamba hatua za haraka zinahitajika kusitisha mapigano katika mji mkuu wa jimbo la Darfur Kaskazini. **PICHA: MTANDAO.**

# Shambulizi la Ukraine laleta maafa Russia

**KYIV, Ukraine**

WIZARA ya Afya ya Russia imesema watu 13 wamejeruhiwa katika eneo la Tver nchini Russia baada ya shambulio kubwa la ndege zisizo na rubani za Ukraine kusababisha moto mkubwa.

Picha ambazo hazijathibitishwa zimeibuka zinazodaiwa kuonesha mlipuko mkubwa katika mji wa Toropets. Huku kanda za video zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zilionesha milipuko na moshi mkubwa angani.

Ilielezwa kuwa maofisa waliamuru watu kulihama eneo hilo baada ya shambulio hilo lililotokea jana asubuhi.

Gavana wa mkoa huo baadaye aliwahimiza wakazi kurejea, akisema kuwa miundombinu yote katika mji ilikuwa ikifanya kazi kama kawaida tena.

Mashirika ya habari ya AFP na Reuters yalinukuu vyanzo vya Ukraine vikisema bohari kubwa la risasi limepigwa na kombora lao.

Ilielezwa kuwa shambulio hilo la kombora lililopiga kwenye ghala la Russia, lilisababisha mlipuko kama wa tetemeko la ardhi na kuwasha moto ambao ulilazimisha kuhamishwa kwa mji katika mkoa wa Tver nchini Russia. Wachunguzi wa tetemeko la ardhi walichukulia tukio hilo kama tetemeko la ardhi, na satelaiti za NASA zilibainisha chanzo kikubwa cha joto katika eneo hilo.

Igor Rudenya, gavana wa eneo la Tver, alisema kwenye mtandao wa Telegram kwamba ndege zisizo na rubani zilitunguliwa na moto uliwaka, lakini hali hiyo ilidhibitiwa.

Reuters ilionyesha kile ilichosema video ambayo haijathibitishwa ya mlipuko wa ghala kwa taasisi ya George William Herbert.

*VOA*

# Somalia yamkamata kiongozi wa al-Shabaab

**MOGADISHU, Somalia**

JESHI la Taifa la Somalia (SNA) limemkamata Ali Geelle, ambaye ni kiongozi mkuu wa kundi la kigaidi la al-Shabaab lenye mafungamano na al-Qaeda, wakati wa operesheni ya kijeshi katika eneo la kati la Galgadud.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Ulinzi ya nchi hiyo.

Taarifa hiyo ilisema kukamatwa huko, kulifanyika katika wilaya ya Galhareeri, mkoa wa Galgaduud, pia kuliwezesha kukamatwa kwa gari, bunduki na risasi, na kwamba Geelle alihusika na unyang'anyi na uhalifu na kuwaunga watoto na kundi la kigaidi.

Jeshi la Taifa la Somalia, likisaidiwa na wanamgambo wa eneo hilo, limekuwa likipigana na al-Shabaab katika majimbo ya kusini kati kwa muda wa miaka miwili na nusu iliyopita, na kukomboa maeneo makubwa ya ardhi, ikiwa ni pamoja na mji wa kimkakati wa pwani wa Haradhere katika eneo la Mudug.

Pia ilielezwa kuwa Somalia imekuwa ikikabiliwa na ukosefu wa usalama kwa miaka mingi, huku vitisho vikuu vikitoka kwa al-Shabaab na makundi ya kigaidi ya Daesh/ISIS.

Ilibainishwa kuwa tangu 2007, al-Shabaab imekuwa ikipigana na serikali ya Somalia na Misheni ya Mpito ya Umoja wa Afrika nchini Somalia (ATMIS), ujumbe wa nchi nyingi ulioidhinishwa na Umoja wa Afrika (AU) na kuongozwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa kundi hilo la kigaidi limeongeza mashambulizi tangu Rais wa Somalia Hassan Sheikh Mohamud kutangaza vita vikali dhidi ya kundi hilo.

*TRT*

**Pia ilielezwa kuwa Somalia imekuwa ikikabiliwa na ukosefu wa usalama kwa miaka mingi, huku vitisho vikuu vikitoka kwa al-Shabaab na makundi ya kigaidi ya Daesh/ISIS.**

# Kuogelea Afrika Mashariki kufanyika Novemba

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya kuogelea ya Afrika Mashariki na Kati yamepangwa kufanyika nchini Burundi kuanzia Novemba 22 mpaka 24 mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa Chama cha Mchezo huo Tanzania (TSA), David Mwasyoge alisema mashindano hayo yatashirikisha vijana wenye umri kuanzia miaka 10.

"Maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri kwa waogeleaji kuendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kuimarisha pumzi zao, sisi tunajiandaa kikamilifu kuhakikisha tunashiriki vizuri," alisema Mwasyoge.

Aidha, alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi za Kenya, Uganda, Ethiopia, Sudani, Rwanda, Djibuti, Tanzania pamoja na wenyeji Burundi.

Alisema kuwa mashindano hayo yatawasaidia kuangalia uwezo wa wachezaji ili waone namna ya kuwaandaa kwa ajili ya kushirki mashindano mbali mbali ya Kimataifa.

Alisema timu tayari imeshachaguliwa na muda wowote kuanzia sasa wataitangaza kusudi wapenzi na wadau wa mchezo huo wafahamu kinachoendelea.

"Timu yetu tutaitangaza muda wowote kuanzia leo ili wadau wetu wafahamu kinachoendelea tunaomba mashiriki, Taasisi na wadau mbali mbali wajitokeze kutuunga mkono ili tufanikishe mipango yetu," alisema Mwasyoge.

# PAMBA JIJI YAWAPOZA MASHABIKI WAKE

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupoteza mchezo kwenye uwanja wa nyumbani CCM Kirumba, jijini Mwanza, Uongozi wa klabu ya Pamba Jiji FC umewapoza mashabiki wake ukiwataka watulie kwa kuwa makocha wanayafanyia kazi mapungufu yaliyoonekana na wanaamini watafanya vizuri kwenye mechi zinazokuja.

Mashabiki wa Pamba Jiji walikuja juu mara baada ya mchezo huo wakidai wachezaji wanacheza kwa kiwango cha chini sana, huku wakitupia lawama upande wa ushambuliaji ambao mpaka sasa hawajafunga bao lolote katika michezo minne waliyocheza.

Jumanne iliyopita, Pamba Jiji ilipata kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Singida Black Stars ikiwa ni cha kwanza kwenye Ligi Kuu.

Meneja wa timu hiyo, Ezekiel Ntibikeha, amewataka mashabiki wa soka mkoani Mwanza kutokata tamaa, badala yake waendelee kuiunga mkono timu yao ambayo bado ni changa kwenye Ligi Kuu.

"Tuwatoe shaka mashabiki wetu, timu itakaa sawa, timu bado ni changa kwenye ligi na mpira una matokeo matatu, kushinda, sare na kufungwa, kama mnavyofahamu ligi hii ni ngumu siyo rahisi kihivyo kama watu wanavyodhani, tunaambiwa ni ligi ya sita barani Afrika kwa ubora, na kweli inaonyesha kile kinachosemwa, hivyo wale wanaoamini kuwa hii siyo Pamba wanayoifahamu waachane na mawazo hayo na wajue tu tunajiweka sawa na tutashinda," alisema.

Alisema wakati mashabiki wao wanalalamika, kuna timu ambazo zimekaa kwenye Ligi Kuu kwa muda mrefu lakini zimeshacheza mpaka michezo mitatu bila kupata ushindi.

"Sisi tumedroo tatu, wenzetu wamefungwa mechi tatu mpaka nne na wapo miaka mitano mpaka sita kwenye ligi hii, wapo pia tuliopanda nao Ligi Kuu hawajapata hata sare, kwa hiyo unaona jinsi ligi ilivyo mgumu, tunaamini huko mbele tutafanya vyema, mashabiki watulie," alisema Ntibikeha



Makamu wa Rais wa klabu ya Yanga, Arafat Ally Haji (kushoto), akimkabidhi jezi ya timu hiyo, Meneja Biashara wa Benki ya NMB Zanzibar, Naima Said Shaame (kulia) baada ya mkutano na waandishi wa habari wa kutangaza wadhamini wa mechi ya marudiano kuwania kufuzu hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE ya Ethiopia. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mtibwa Sugar kufungua Ligi ya Championship leo

**Na Adam Fungamwango**

LIGI ya Championship inatarajiwa kuanza leo kwenye viwanja viwili nchini huku Mtibwa Sugar ambayo ilishuka daraja msimu uliopita ikifungua pazia kwa kucheza na Green Warriors kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani, Morogoro.

Wakati Mtibwa ikiwa nyumbani leo, mechi nyingine ya ufunguzi wa ligi hiyo ambayo inasaka timu mbili zitakazopanda moja kwa moja Ligi Kuu msimu ujao, kwenye Uwanja wa Sokoine kutakuwa na mechi nyingine, Mbeya City itakapokuwa nyumbani kukipiga dhidi ya Bigman FC ambayo zamani ilijulikana kwa jina la Mwadui FC.

Baada ya michezo hiyo miwili ya ufunguzi leo, Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa michezo mingine ambapo timu nyingine iliyoshuka Ligi Kuu msimu uliopita, Geita Gold nayo itakuwa nyumbani, Uwanja wa Nyankumbu, Geita itakapokipiga dhidi ya TMA, Cosmopolitan itaialika African Sports, Uwanja wa Mabatini, wakati kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea, wenyeji Songea United wataumana na Mbeya Kwanza.

Mechi zingine tatu za kumalizia raundi ya kwanza zinatarajiwa kupigwa Jumapili wakati Polisi Tanzania itakapocheza dhidi ya Mbuni FC, Uwanja wa Ushirika, Moshi.

Biashara United itakuwa kwenye Uwanja wa Karume, Musoma Mkoani Mara kuwaalika Transit Camp, huku Kiluvya FC ikiwa Mabatini, Mlandizi itacheza na Stand United.

Baada ya michezo hiyo, ligi itaendelea tena Septemba 27 kwenye viwanja mbalimbali.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### REAL MADRID WAMTAKA SALIBA
KLABU ya Real Madrid ilituma skauti katika mchezo wa Desby ya London  Kaskazini Jumapili iliyopita kumfuatilia nyota wanayemuwinda kutoka Arsenal,  William Saliba na beki wa kati wa Tottenham na Argentina, Cristian Romero mwenye miaka 26. ***(Defensa Central)***

### AC MILAN YAMTAKA CHUKWUEMEKA
WINGA wa Chelsea mwenye umri wa chini ya miaka 20, Carney Chukwuemeka ni miongoni mwa walengwa wa AC Milan katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Calciomercato)***

### DAVIES AKARIBIA KUTUA R. MADRID
REAL Madrid wanakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mlinzi wa Bayern Munich, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 23, kwa uhamisho wa bila malipo. ***(AS)***

### LIVERPOOL YAMTOKEA MACHO BADE
LIVERPOOL inataka kumsajili beki  wa Sevilla,  Mfaransa Loic Bade mwenye  wa miaka 24, huku wakifikiria kumfanya mbadala wa mlinzi wao wa kati wa Uholanzi Virgil van Dijk mwenye miaka 33. ***(Caught Offside)***

### OSIMHEN BADO ATAJWA CHELSEA
CHELSEA inaweza kurejea kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25 Januari kutokana na kipengele cha mauzo katika mkataba wake wa mkopo huko Galatasaray. ***(Football Insider)***

### BARCA WALIKATAA KUMUACHIA YAMAL
BARCELONA ilikataa ofa ya takribanI pauni milioni 210 kutoka kwa Paris St-Germain kwa ajili ya winga wa Hispania, Lamine Yamal mwenye umri wa miaka 17  mwezii Juni, kwa mujibu wa Andy Bara , wakala wa kiungo wa kati wa Barca na Hispania Dani Olmo. ***(Mundo Deportivo)***

### MATIP ATAKIWA WEST HAM BURE
KLABU ya West Ham inaendelea kufanyia kazi mpango wa kumsajili beki wa zamani wa Cameroon, Joel Matip mwenye umri wa miaka 33, kwa uhamisho wa bure. ***(Football Insider)***


### RABIOT APANGA KUIGOMOEA JUVENTUS
MAMA na wakala wa Adrien Rabiot amesema kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29, ambaye amekuwa akihusishwa na Newcastle United na Manchester United, hatarejea klabu ya zamani ya Juventus. ***(Mirror)***

### EVERTON KUNUNULIWA HIVI KARIBUNI
MFANYABIASHARA wa Marekani, John Textor ana imani kuwa dili la kuinunua Everton linaweza kukamilika baada ya wiki nne. ***(Guardian)***

### KOCHQ MONGAN ATOSWA REAL MADRID
ANDY Mangan wa Stockport County amezuiwa kujiunga na timu ya makocha ya Real Madrid baada ya kunyimwa kibali cha kufanya kazi kwa sababu ya kanuni za Brexit. ***(Times)***

### CHUKWUEMEKA KWA MIKOPO UTURUKI
KLABU ya Galatasaray ina nia ya kumsajili winga wa Chelsea mwenye umri wa miaka 20 kutoka England, Carney Chukwuemeka kwa mkopo.***(Teamtalk)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE BRUYNE HATIHATI KUIVAA ARSENAL

Mbelgiji huyo alitolewa uwanjani wakati wa mapumziko kwenye mchezo dhidi ya Inter Milan na sasa ana......

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola ameonesha wasiwasi wake juu ya kiungo wake, Kevin De Bruyne kama atakuwa sehemu ya kikosi kitakachoivaa Arsenal kwenye Uwanja wa Etihad siku ya Jumapili baada ya Mbelgiji huyo huyo kulazimika kutoka nje baada ya kuumia kwenye mchezo dhidi ya Inter Milan juzi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

De Bruyne alitolewa wakati wa mapumziko wakati wa sare ya bila kufungana Jumatano usiku.

Mbelgiji huyo alipata jeraha mwishoni mwa kipindi cha kwanza baada ya kujaribu kukimbilia mpira wa pasi ya Jack Grealish.

"Tutafanya tathmini na nitakuwa na taarifa zaidi," alisema Guardiola.

„Madaktari waliniambia hakuwa sawa kucheza lakini nilikuwa nikifikiria kumbadilisha wakati wa mapumziko.

"Unapokuwa peke yako na kupoteza mipira rahisi, ni shambulio la kukabiliana, haiwezekani kulizuia. Unapaswa kuwa sahihi zaidi. Ilifanyika hasa upande wa kushoto na Kevin alipitia wakati huo. Tulipoteza mpira bila shinikizo.

Licha ya kuanza kampeni ya Ligi ya Mabingwa kwa sare, Guardiola alisisitiza kuwa alifurahishwa na uchezaji wa timu yake.

Inter walipata nafasi, lakini pia timu ya Guardiola ilijumuisha mipira miwili ya kichwa ya dakika za lala salama kutoka kwa mchezaji wa akiba Ilkay Gündogan.

"Ni mwanzoni mwa msimu," alisema bosi huyo wa Man City.

"Mashindano yatakuwa bora, kwa muda zaidi tutakuwa bora. Tumecheza vizuri sana. Naipenda timu yangu, sisi ni timu ya ajabu. Inter ni timu ambayo inajilinda vizuri."

Nafasi nzuri ya Inter iliangukia kwa kiungo wa zamani wa Manchester United, Henrikh Mkhitaryan, ambaye alipiga shuti juu ya lango la goli kutoka ndani ya eneo la hatari.

# ENRIQUE: MFUMO MPYA UEFA NI MGUMU

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Luis Enrique alisema "kutojulikana" kwa muundo mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ilifanya iwe vigumu kufurahia ushindi wa kwanza wa timu yake dhidi ya Girona Jumatano iliyopita.

PSG walipata ushindi baada ya kipa wa Girona, Paulo Gazzaniga, ambaye alizuia juhudi nyingi za mabingwa hao wa Ufaransa, kufanya makosa makubwa dakika za mwisho za mechi na kuwapa wenyeji ushindi wa bao 1-0.

Lakini zikiwa zimesalia mechi saba kumalizika kwa kile kinachoitwa awamu mpya ya ligi ya mashindano hayo, kocha huyo wa PSG alisema huenda ikachukua muda kufahamu umuhimu wa ushindi wa timu yake.

"Kushinda mechi au taji lolote ni ngumu, lakini hatujui ukubwa wa shindano hili na muundo huu," alisema Luis Enrique.

"Tutalazimika kucheza mechi dhidi ya timu ambazo zina ratiba rahisi kuliko yetu, tutahitaji pointi ngapi?

"Kuna mambo mengi yasiyojulikana ambayo yanahitaji kusafishwa."

Chini ya muundo mpya wa Ligi ya Mabingwa, timu hucheza mechi nane dhidi ya wapinzani nane tofauti, huku timu nane za juu katika ligi ya timu 36 zikifuzu moja kwa moja hadi 16 bora, na 16 zinazofuata zikicheza raundi nyingine ya mtoano.

PSG walitawala mchezo kwa muda mrefu, lakini timu ya mwaka jana iliyoshangaza kwenye LaLiga iliweka mchezo sawa hadi dakika za lala salama, wakati shuti la Nuno Mendes lilipotoka katikati ya miguu ya Gazzaniga.

"Nadhani tulikuwa bora, lakini Girona alituchezesha kwenye duru na kututia kizunguzungu," alisema Enrique.

"Wakati wa mapumziko, tulisema kwamba ikiwa hatungeshinikiza, tungeteseka. Ilibidi tushinde, na ilikuwa ngumu sana."

"Ilikuwa ngumu sana. Nilimwambia kocha wa Girona, Michel kwamba hii ilikuwa mbaya zaidi."

Licha ya ushindi huo, PSG ilipata shida huku mshambuliaji Marco Asensio akichechemea kabla ya muda wa mapumziko.

"Alihisi kutetemeka. Marco alikuwa ameanza msimu vizuri. Hili ni soka la kulipwa na tuna kikosi kizuri sana," alisema kocha huyo wa zamani wa Barcelona.

PSG itacheza na Reims ugenini kwenye Ligue 1 Jumamosi, huku Girona ikisafiri kwa mechi ya LaLiga dhidi ya Valencia.



## Ibrahimovic: Mimi ndio bosi wa AC Milan

**MILAN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa zamani wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic alizungumzia jukumu lake kuu katika klabu hiyo ya Italia baada ya kufungwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool akisema "wengine wanafanya kazi kwa ajili yangu."

Wamiliki wa Milan, RedBird Capital, walitangaza mnamo Desemba 2023 kwamba Ibrahimovic alijiunga kama mshirika wa uendeshaji na kuwa mshauri mkuu wa klabu.

Nyota huyo wa Sweden alitangaza kustaafu soka mwishoni mwa msimu wa 2022-23 baada ya kuzichezea Milan, Ajax, Juventus, Inter Milan, Paris Saint-Germain, Manchester United, Barcelona na LA Galaxy.

Alipoulizwa na Sky Sport kufafanua jukumu lake, Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 42, alisema: "Mimi ndiye bosi na ninaongoza, wengine wote wananifanyia kazi."

Ibrahimovic aliendelea kujibu swali kuhusu ukosoaji wa kazi yake kutoka kwa mkurugenzi wa zamani wa klabu hiyo, Zvonimir Boban.

"Simba anapoondoka, paka hufika. Simba anaporudi, paka hupotea," alisema Ibrahimovic.

"Kiwango ni cha chini sana, kuna mazungumzo mengi lakini nafikiria kufanya kazi tu. Nilikuwa mbali kwa sababu za kibinafsi, lakini nimekuwa hapa tangu siku ya kwanza."

Ibrahimovic alizungumza pia kuhusu biashara ya uhamisho ya Milan katika dirisha la majira ya joto.

"Iliendа kama tulivyotaka, kila kitu tulichotafuta na kukosa tulipata. Wa mwisho alikuwa Tammy Abraham, kutoa uimarishaji wa ziada katika mashambulizi."



## Odegaard pigo kwa Arsenal

**LONDON,** England

NAHODHA wa Arsenal, Martin Odegaard atakuwa nje "kwa muda" baada ya kupata jeraha kubwa la kifundo cha mguu alipokuwa akiichezea Norway wiki iliyopita, kocha Mikel Arteta amesema.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alipiga shuti wakati wakifungwa na Austria kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa mjini Oslo Septemba 9 na kurejea London akiwa na magongo.

Ødegaard alikosa mechi ya Jumapili ya London Kaskazini dhidi ya Tottenham Hotspur.

"Uchunguzi ulionesha kuwa amepata majeraha fulani haswa kwenye moja ya mishipa kwenye kifundo cha mguu," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

"Ni kitu muhimu sana kwa hivyo tutampoteza kwa muda."




Arteta, ambaye timu yake iko nafasi ya pili kwenye ligi na pointi mbili nyuma ya Manchester City, alisema anatumaini haitachukua miezi "lakini wacha tuone."

Ødegaard amekuwa mchezaji muhimu kwa Arsenal, akikosa mechi chache tu katika misimu mitatu iliyopita, na kutokuwepo kwa muda mrefu kutakuja kama pigo kubwa.

"Yeye ni nahodha wetu. Amekuwa mmoja wa wachezaji wakubwa na bora katika timu yetu," alisema Arteta.

"Utambulisho wetu unahusishwa sana na jinsi anavyocheza na tabia yake, ni mtihani mkubwa kwa timu kuona jinsi tunavyoweza kuonesha sura tofauti," alisema.

HABARI MICHEZO

# KOCHA MGUNDA ANUKIA KENGOLD

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa zamani wa klabu ya Simba, Juma Mgunda anatajwa kuwa mmoja wa makocha 10 waliopeleka wasifu wao kwenye klabu ya KenGold kutaka kuirithi kazi ya Fikiri Elias aliyejiuzulu wiki hii kwa kile alichodai kushindwa kutimiza malengo.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa tayari makocha mbalimbali nchini wameshapeleka maombi ya kuitaka kazi hiyo, akiwemo Mgunda ambaye hivi karibuni alimaliza mkataba na klabu ya Simba akiwa amezifundisha timu za wanaume na wanawake.

Taarifa zinasema kuwa baadhi ya makocha ambao wametuma wasifu wao kutaka kuifundisha timu hiyo iliyoanza kucheza Ligi Kuu msimu huu ni pamoja na Zuberi Katwila, Fransis Baraza, Malale Hamsini na Mrundi, Haruna Hermana.

Hivi karibuni pia kulikuwa na taarifa ya Mgunda kutakiwa na Namungo baada ya timu hiyo kuwa na matokeo yasiyoridhisha kwenye Ligi Kuu huku kukiwa na tetesi za kutaka kuachana na kocha wake Mwinyi Zahera.

Kocha Elias alijiuzulu Jumatatu iliyopita mara baada ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC na kuchapwa bao 1-0, mchezo huo ulichezwa Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

"Nilijiwekea malengo kuwa nisipopata pointi sita katika michezo minne basi nitajiuzulu, sasa tayari mchezo wa tatu hatujapata pointi hata moja, na hata kama nikiendelea na kushinda tunakuwa na pointi tatu. Mimi kama mwana taaluma, nimefanya hivi kulinda taaluma yangu pamoja na uwajibikaji," alisema kocha huyo wakati akitangaza kujiuzulu.

Kilikuwa ni kipigo cha tatu mfululizo kwa timu hiyo ambayo mwanzo ilichapwa mabao 3-1 dhidi ya Singida Black Stars, ikafungwa mabao 2-1 dhidi ya Fountain Gate, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati Mkoani Manyara, kabla ya kipigo cha tatu kilichomfanya kocha huyo ajiuzulu.



Wachezaji wa Azam FC wakishangilia moja ya bao walilofunga jana kwenye mchezo dhidi ya KMC katika uwanja wa Manispaa ya Kinondoni, Mwenge Jijini Dar es Salaam, Azam iliibuka na ushindi wa mabao 4-0. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waamuzi wanne wasimamishwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAAMUZI wanne wanaochezesha Ligi Kuu ya Zanzibar wamesimamishwa katika ratiba ya waamuzi kwa mizunguko mitano baada ya kushindwa kutafsiri na kusimamia Sheria 17 za mpira wa miguu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamati ya Uendeshaji na usimamizi wa Ligi hiyo, waamuzi hao waliruhusu KMKM kuchezesha wachezaji 12 kwa muda wa dakika nne wakati timu hiyo ilipocheza na Muembe Makumbi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa adhabu hiyo imetolewa kwa mujibu wa sura ya 27 kifungu cha tatu ibara ndogo ya pili na tisa ya kanuni ya mashindano.

Waamuzi walikumbana na adhabu hiyo ni mwamuzi wa kati Haji Nyonje na wasaidizi wake Yussuf Issa Shombe na Ismail Masoud Bakar na mwamuzi mezani Hamiar Muhsin Kamara wa mezani. Hivyo kamati hiyo inawashauri waamuzi hao kufuata kanuni na Sheria za soka, kuwa na utimamu na umakini wakati wa utekelezaji wa majukumu yao, ili kulinda heshima ya mpira wa Zanzibar na makosa yasijirejee.

Sambamba na hayo kamati hiyo imetoa onyo kwa waamuzi Rashid Farahan, Haji Nyonje na Hamiar Muhsin Kamara kwa kushindwa kuwasilisha ripoti ya mchezo waliochezesha na kutojazwa kikamilifu na unadhifu na kwa waliotakiwa kuwasirisha ripoti ya mchezo kiny-

## Al Ahli Tripoli wakodi mabaunsa

INATOKA UK. 24

su bao hasa tukiwa bado hatujapata mabao itatuweka kwenye presha, ni lazima sisi tuwe wa kwanza kupata goli na kuendelea kuumiliki mchezo," aliongeza kusema.

Alisema kwa sasa hana wasiwasi sana na safu yake ya ulinzi, lakini anachofanya ni kuitengeneza safu ya ushambuliaji inayoongozwa na Leonel Ateba ili kuhakikisha inapata mabao mengi iwezekanavyo.

"Ili tufuzu makundi tunahitaji ushindi, na ili tushinde tunahitaji mabao, safu ya ushambuliaji ni lazima ihakikishe inafunga mabao na hilo ndilo ninalotilia mkazo mazoezini mara baada ya kumalizika kwa mchezo wetu wa kwanza kule Libya," alisema kocha huyo, raia wa Afrika Kusini.

Mchezo huo wa marudiano umepangwa kuanza saa 10:00 jioni kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa huku Simba ikihitaji ushindi wa aina yoyote kuweza kutinga hatua ya makundi

## NMB yachochea moto mchezo wa Yanga, CBE

INATOKA UK. 24

wako hapo.

Awali, akimkaribisha Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Yanga, Ali Kamwe, aliwashukuru NMB na wadhamini wenza kwa kuchagua kushirikiana na timu yake katika kuipa nguvu kuelekea hatua ya makundi ya michuano hiyo.

"Tunawashukuru NMB na wadhamini wengine wote waliowezesha wiki hii yote ya kujiandaa kuelekea mechi hii, mmeiheshimisha Yanga, kwani kabla hatujahesabu mauzo ya tiketi zetu za mechi, tayari tushaingiza zaidi ya Sh. Mil. 200 kutoka kwa wadhamini wetu hawa tu," alitamba Kamwe.

Alibainisha ya kwamba ratiba ya matukio kwa Ijumaa hii yatafunguliwa kwa dua maalum itakayosomwa katika Madrassat Swifatul Nnabawiyah iliyopo Kilimani kwa Msolopa, Zanzibar asubuhi na baada ya Swala ya Ijumaa, watatoa misaada kwa Watoto Yatima visiwani hapa.

"Tayari kikosi chetu chote kimetua Zanzibar kasoro Farid Mussa tu ambaye ni majeruhi na sababu za kusafiri na kikosi chote ni kundelea kujiandaa na mechi za ligi kuu zinazofuata, tuna ratiba ngumu mno ambayo hairuhusu mchezaji yeyote kuachwa mbali na kikosi," alisema Kamwe.

Yanga inahitaji sare au ushindi wowote kuweza kufuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa Jumamosi iliyopita kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

Michezo
Ijumaa Septemba 20, 2024
Nipashe

## Enrique: Mfumo mpya Uefa ni mgumu

UKURASA 22





# Al Ahli Tripoli wakodi mabaunsa

●●● Waogopa kufanyiwa kile walichowafanyia Simba Libya, Fadlu asema haitowasaidia kwa kuwa....

Wachezaji wa Simba, Awesu Awesu (kulia) na Yusuph Kagoma wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo jana kujiandaa na mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali inayoonesha wapinzani wa Simba, Al Ahly Tripoli wameingiwa na woga wa kufanyiwa kile walichowafanyia wekundu hao kwenye mchezo wa kwanza Libya, wamelazimika kukodi walinzi binafsi (Bodyguard) kwa ajili ya kuwalinda.

Mashabiki, wachezaji na baadhi ya Maofisa wa klabu hiyo walionekana kuwafanyia vurugu wachezaji wa Simba pamoja na waamuzi wakati na baada ya mchezo huo uliomalizika kwa suluhu.

Timu hiyo iliwasili jana jijini Dar es Salaam, tayari kwa mchezo wa marudiano, Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jumapili.

Mabaunsa hao wa hapa nchini walionekana kuwalinda wachezaji na viongozi kuanzia Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere kwa chochote kibaya kitakachotokea, ingawa nyuso za wageni hao zilionekana kuwa bado zina hofu.

Wakati timu hiyo ya Libya ikifanya hivyo, Kocha Mkuu wa Simba, David Fadlu, amesema ameshaiandaa vyema timu yake kwa ajili ya kuhakikisha inapata ushindi licha ya kuonekana mechi hiyo ina mambo mengi.

Fadlu, alisema matokeo ya mchezo uliopita wameyaweka pembeni na wanaelekeza nguvu na mawazo yao kwenye mchezo huo wa Jumapili huku wakijipanga kwa ajili ya ushindi.

"Tuko nyumbani, sasa tunatakiwa tuwe makini kwani tunacheza mbele ya mashabiki wetu ambao hawana wanachohitaji zaidi ya ushindi, wao (Al Ahly Tripoli) wafanye wanachotaka kukifanya, sisi tupo tayari uwanjani, lengo letu ni ushindi tu" alisema Fadlu.

Alisema pamoja na kwamba wanahitaji ushindi lakini mpango mkakati wa kulinda bado utaendelea kwani anatambua kuwa wapinzani wake watakuja kwa kushambulia sana ili wapate bao moja ambalo litawaweka salama kwenye mchezo huo.

Alisema wamejipanga kupata mabao ya mapema ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kushika mchezo huo.

„Kama tukifanya makosa ya kuruhu-

INAENDELEA UK. 23

## NMB yachochea moto mchezo wa Yanga, CBE

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAKATI kikosi cha Yanga kikiwasili salama jana visiwani hapa kwa ajili ya mchezo wao wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE ya Ethiopia, benki ya NMB imekoleza moto kuelekea mchezo huo baada ya kutangaza kudhamini mtanange huo.

Yanga wanashuka uwanjani kesho saa 2:30 kuumana na mabingwa hao wa Ethiopia huku wakiitambulisha NMB kama mmoja wa wadhamini wa mchezo huo wakiupa jina la ‚Timu Bora, Benki Bora'.

Akizungumza kwenye hafla ya utambulisho wa udhamini huo, Meneja Biashara wa benki hiyo Zanzibar, Naima Said Shaame, alisema siri ya uamuzi wao wa kujitosa kuidhamini Yanga ni mvuto ilionao klabu hiyo, unaoakisi mafanikio makubwa katika soka kitaifa na kimataifa.

"Tumevutiwa na mafanikio ya klabu hii, tukaona ipo haja ya Timu Bora kupewa nguvu na Benki Bora. Wametoka kutwaa Ngao ya Jamii katika ufunguzi wa msimu huu, lakini katika Ligi ya Mabingwa Afrika, wamefuzu raundi hii kwa kishindo baada ya kuwachapa Vital'O ya Burundi kwa jumla ya mabao 10-0.

"Kwa kutambua ukubwa wa Yanga, tukalinganisha na ukubwa wa NMB, tukaona ipo haja ya kuwasapoti katika mechi dhidi ya CBE itakayopigwa hapa wikiendi hii na leo (jana) tuko hapa kutambulishwa rasmi kama washirika wa Yanga kuelekea mechi hii," alisema Naima.

Alibainisha ya kwamba, ushirikiano baina ya benki yake na Yanga umeshaanza katika kuhanikiza wiki nzima na wanaamini mchango wa taasisi yake utakuwa chachu ya Yanga kushinda mechi hiyo na kufuzu hatua ya makundi kwa mara tatu katika historia yao.

"Nitumie nafasi hii kuwakumbusha mashabiki wa Yanga kuwa, huu sio mwanzo, kwani tunafanya kazi na Yanga katika maeneo mbalimbali ikiwemo usajili wa wanachama kupitia kadi tofauti tofauti. Ukiona Tawi la NMB, maana yake umeiona Yanga na unaweza kusajili uanachama

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >